# *ISHARA YA KWELI ILIYOPUUZWA*

Kukusanyika asubuhi ya leo katika Jina la Bwana Yesu, na baada ya kuomba sana. Na asubuhi ya leo, sikuamka mapema. Kidogo nilikuwa nimechelewa, kuamka, na ninadhani kila mtu anajua ni kwa nini hivyo, sasa hivi.

2 Nilikuja nyumbani, hivi majuzi asubuhi, ama hivi majuzi usiku, naye jirani yangu alikuwa amesimama uani, yeye na binti yake mdogo. Mkewe ni nesi katika chumba cha kujifungua huko hospitalini. Kwa hiyo alikuwa na—na fimbo mkononi mwake, yapata urefu *huu*, yenye ma—maandishi madogo juu yake, utepe fulani, na kitu kidogo kilichosema, "Babu Branham kwenye, ninaamini, ama saa 9:43 au 10:43, Oktoba 11." Halafu, maandishi makubwa sana kwenye mabano huku chini, yaliyosema, "Wewe ni mzee zaidi kuliko unavyodhania." Kwa hiyo nina haki za kisheria sasa kupumzika kidogo zaidi asubuhi. Hiyo ni kweli, Ndugu Wright, wakati unaponinii—wakati unapokuwa babu?

3 Na kwa hiyo nadhani hilo kwa namna fulani linanipa udhuru, basi, Dada Kidd, asubuhi ya leo, kutokuwa nimeamka wakati ulipotoka Ohio. Hakika ninajisikia mzee zaidi kwa miaka kumi, nafikiri, hata hivyo, baada ya hilo. Lakini, kama nyote mjuavyo ya kwamba nina mjukuu mdogo huko nje, mwenye uzito wa karibu ratili saba ama nane, kitu kama hicho, kitoto chenye sura mbaya kuliko vyote nilivyopata kuona. Kasema, "Anafanana kabisa na babu yake." Kwa hiyo. . . Nami nilikuwa tu nikiona mahali alipoenda, mahali Billy alipoenda.

4 Kwa hiyo, jana usiku, nikishuka kuja kwenye ukumbi, baada ya kupiga simu zangu, nilikutana na kundi la marafiki waaminifu kutoka Georgia na huku karibu, nasi sote tulikuwa huko nje tukiwaangalia hao jamaa wadogo. Nao wanapendeza. Sasa, hao wananinii tu. . . Daima nilihisi kitu kama, "Billy, unaogopa utawavunja, mwajua. Hao ni wadogo sana." Nami naamini ilikuwa ni Dada Beeler aliyesema. . . Nilikuwa nikiwazia. . . Alikuwa akiwazia hivyo pia, lakini, baadaye, alikuta kwamba hawavunjiki kwa urahisi hivyo. Kwa hiyo, nafikiri hiyo karibu ni kweli.

5 Jana alasiri nilikuwa na majaliwa ya kuwa nyumbani mwa dada yetu hapa wa kanisa hili, nyumbani mwa binti yake; nami nafikiri yeye pia yumo humu kanisani, ambapo walikuwa na karamu ndogo ya siku ya kuzaliwa kwa Ndugu Neville. Naye alipita siku nyingine ya kihistoria jana. Na kwa hiyo tunamwambia Ndugu Neville, "Heri za siku ya kuzaliwa," kila mmoja wetu, kwa kuwa ni ndugu mzuri sana. Na, hakika, ndiyo kwanza apite ishirini na mitano, kidogo, kwa hiyo basi ni kama mimi. Na kwa hiyo ndiyo kwanza tuupite, mara ya pili. Jambo

ndilo hilo. Sasa hiyo ni kuwa mzee, wakati unapopita alama hiyo mara ya pili, mwajua.

6 Ninakumbuka ile asubuhi ambayo Frankie Weber alikuja hapa. Naye alikuwa ni jirani wetu wa karibu hapa; binti yake anaishi pale sasa. Yeye yuko Florida. Na mimi na Frankie tulisoma pamoja. Basi Frankie alitoa matoleo ya siku yake ya kuzaliwa. Nami nilikuwa nikihubiri wakati huo yapata miaka mitatu ama minne. Nilimwongoza Frankie kwa Bwana Yesu. Ndipo akatoa robo. Nafikiri nilikuwa na miaka ishirini na miwili. Basi akatoa robo. Nikawazia, "Loo, jamani, unataka kuniambia ya kwamba Frankie Weber ana umri wa miaka ishirini na mitano? Whiu! Jamani, ninahofia wakati nitakapofikia miaka ishirini na mitano." Sasa ninakaribia kuweka tatu za hizo, kwa hiyo basi, hivi karibuni sana. Kwa hiyo haichukui muda mrefu kupita.

7 Ninapoangalia hapa na kumwona Ndugu na Dada Kidd katika umri wa miaka themanini na kitu na huku wanazidi kuwa wenye nguvu, nafikiri, "Bwana Yesu, nisamehe kwa kunung'unika, kwenye umri wa miaka hamsini na miwili." Nao. . . Una themanini, na Ndugu Kidd ana themanini na mmoja. Hiyo ni kweli? Themanini na mmoja. Nao wangali katika huduma. Nawaambia, hilo linatupa ujasiri. Sivyo? Hakika linatupa. Bwana hakika ni mwema kwetu.

8 Sasa, kuna jambo moja tu baya ninaloogopa, kufanya mkutano hapa asubuhi, na hiyo ni. . . Ni baya sana, linasikika kama jambo baya sana la kusema. Lakini nina marafiki wengi sana ambao huja, kutoka mbali sana, kwenye—kwenye ibada.

Siwaoni akina Evans hapa, bali wako hapa mahali fulani, nadhani. Kamwe hawakosi hata mmoja. Nanyi mnajua ni maili ngapi wanazoendesha gari kila Jumapili kusikiliza mahubiri? Maili elfu moja mia tatu. Hawawezi kufanya safari hiyo kwa chini ya dola sitini hadi sabini kwa juma, kwenda kanisani, hiyo ni kweli, wakati wanapokuja hapa pamoja na yote, familia yao, wanaenda huku, wanalipia.

9 Sasa, si hivyo tu, lakini huyu hapa maskini ndugu mmoja kutoka huko Alabama, anaendesha gari karibu umbali huo kila juma. Ndugu. . . Loo, jamani! Ndugu "Welt"? [Ndugu mmoja anasema, "West."—Mh.] West. Yeye anaonekana kama mvulana, kwangu mimi. Yeye ni—yeye ni baba, ana watoto chungu nzima. Lakini daima hunikumbusha tu, yeye anaonekana kijana sana, yeye na mke wake. Ndugu West.

10 Ndugu na Dada Palmer wanaoketi kule nyuma, kutoka huko chini ya Macon, Georgia.

Na—na Dada Ungren, wao kwa kawaida huwa hapa, kutoka huko chini, Memphis, Tennessee. Je! wako hapa asubuhi ya leo? Mimi—mimi . . . Kwa kawaida wao huwa hapa. Dada Ungren na—

na lile kundi kutoka huko Memphis, Tennessee, huko, naam, huko nyuma kabisa.

Na wapo wengine. Ninaninii tu. . . Wao ni wengi sana, kuwataja. Baadhi yao, huko chini kabisa Kentucky ya kusini. Baadhi yao, huko mbali sana karibu na Chikago. Na wengine wanatoka Chikago, na juu ya Chikago, kotekote huko.

11 Jumapili, nilisikia kulikuwako na mtu hapa kutoka mbali huko Kalifornia, alikuwa na muda kidogo tu wa kukaa; alitaka kuniona. Hakika, nilikuwa na shughuli nyingi sana, baada ya mkutano. Ndipo mtu huyo akarudi, bila ya mimi kumwona.

Mwingine akaja kutoka huko, Illinois, mahali fulani. Ikiwa mtu huyo yupo hapa asubuhi ya leo: hayo yalikuwa ndiyo matofaa mazuri kuliko yote niliyopata kula. Naye aliniletea pishi la matofaa.

Na mmoja wa ndugu kutoka huko chini Georgia, ninaamini ilikuwa, ama mahali fulani, alileta furushi kubwa mno la mapekani, kubwa karibu *hivi*, maganda ya makaratasi. Na, loo, kweli ninaweza kuyala!

12 Sasa hivi, hakika, sili vyakula vitamu siku hizi, sijavila tangu mama yangu alipotuacha. Ninamtafuta Bwana nipate ono jipya. Nala tu vitu vyepesi, kiasi kidogo tu ninachoweza kuishia; nimepoteza ratili ishirini za uzito. Ambazo ni. . . Sasa, sifungi. Mimi. . . La, la. Hiyo, kufanya tu jambo hilo, hiyo si kumpa Bwana hayo. Unataka kumpa Bwana yaliyo bora sana uliyo nayo. Si ninii. . .

13 Ilitokea kwamba nilimwona Ndugu Sumner na hao wengine huko nyuma pia. Kuna wengi sana. Mimi. . .

Kama vile, Jumapili iliyopita, nilikuwa nikiwataja watu ambao—ambao walikesha pamoja na mama, na kadhalika. Na dada mwaminifu kweli alikuwa pale. Nilisahau kulitaja jina la mwanamke huyo. Sasa, kama yupo hapa asubuhi ya leo, ninaomba msamaha. Mmoja wao alikuwa ni Dada Beeler, na huyo mwingine alikuwa ni Dada na Ndugu Stephie. Na wengi sana! Mimi. . .

14 Nyote mnanijua vizuri vya kutosha kujua ya kwamba silimaanishi, wakati ninapoliacha jina ama kutomtaja mtu. Jinsi wote walivyokuwa waaminifu! Na wakati mwingine nikiketi tu hapa, nitamtaja mtu fulani ndio kwanza anaingia niani mwangu. Lakini mimi. . . Kwa jambo hilo, ninamaanisha kundi lote, kila mtu, mnaona, ni vema tu kabisa. Halafu basi, kila mtu, anapendeza sana, ni mwema kwetu. Nasi hakika tunalifurahia hilo.

15 Na sasa, asubuhi ya leo, tutajaribu kulikaribia Neno la Mungu tena. Sasa, ningetaka kutoa tamshi hili, kusudi liwe dhahiri kabisa, ya kwamba si—siji tu kwenye mkutano wowote nipate tu kuonekana. Siji huko kusema tu, "Vema, nataka labda

kumwomba Mungu anipe U—Ujumbe ambao utawafanya tu watu kujisikia vizuri sana na kupaza sauti." Tumekuwa na mengi sana ya hayo, lakini, nasi tunafurahia hilo. Hilo ni sawa. Mnaona? Hilo ni zuri sana. Mnaona? Bali ninalotaka kujua, ni, "Bwana, Wewe yaongoze mawazo yangu kwenye jambo fulani litakalokuwa ni msaada kwa watu, ambalo litawaweka karibu zaidi na Mungu, ambalo—ambalo—ambalo litawafanyia jambo fulani." Kwamba, kwamba sio zaidi sana kuwajenga kiroho, bali kuwajenga katika maarifa na maonyo ya Mungu, ili kwamba wajue jinsi ya kusimama adui anapokuja.

16 Nilikuwa nikizungumza na dada mmoja ambaye amekuwa huku akitutembelea juma hili, Dada Palmer. Akasema, alitaka kujua jinsi nilivyopata kuishi kwenye nchi hii. Ni, unaingia tu humu ndani, na, naam, kila ninapofika bondeni ninakuwa mgonjwa mara tu ninapoingia. Bonde hili hapa kweli linaleta magonjwa. Tunajua hilo. Lakini Mungu anao watoto wengi sana huku chini. Na kwa hiyo moja ya siku hizi . . .

17 Ninamtafuta Bwana sasa, kupata Ujumbe halisi wa moja kwa moja kutoka kwa Mungu. Mnaona? Nami, kwa msaada wa Mungu, ninakusudia kushikilia tu mpaka Yeye atakapokuja, hiyo ni mpaka atakaponitolea matamshi fulani. Kwa kuwa ninajisikia ya kwamba kunapaswa kuweko . . . Kuna jambo fulani lililo karibu kutukia karibu na hapa, nami ninataka kujua ni kitu gani. Ninataka kujua moja kwa moja kutoka kwa Mungu, kusudi niweze kusema ni BWANA ASEMA HIVI. Mnaona? Halafu basi—basi mnaweza, ninyi, watu, basi mtajua ya kwamba sio mimi. Kwa hiyo, nataka kujaribu kulifanya hivi kwamba, kwamba, ama, kusikia kutoka Kwake kwanza.

18 Maana, kama Yeye akiweka Maneno Yake ndani—ndani ya mtu, vema, basi si mtu huyo tena; ni Yeye. Basi kama mtu huyo anayasema, kwa nafsi yake, basi hayatafaa kitu hata hivyo. Lakini kama Yeye ni, Neno la Bwana, limo ndani ya huyo mtu, Litatokea, halafu litakuwa—litakuwa ni la kweli kabisa. Hivyo ndivyo tulivyoagizwa. Katika Biblia, kwenye yapata mlango wa 20 wa Kumbukumbu la Torati, ninaamini, lilisema, naam, "Angalieni, na kama mtu akinena kwa Jina la Bwana, wala lisitimie, basi msimjali mtu huyo." Mnaona? "Bali kama wakilisema nalo linatimia, basi ni afadhali mlisikie, mnaona, kwa kuwa linatoka kwa Mungu."

19 Hivyo ndivyo Mungu amefanya. Yeye ameweka mpango Wake wa kawaida hapa katika Biblia. Tunajua jinsi ya kusoma huo. Lakini yapo mambo mengine, ambayo—ambayo kwa Kanisa na wakati na kadhalika, ambayo Yeye hajayaandika hapa katika Biblia, kwa hiyo Yeye huiweka Sauti Yake katika mtu mmoja nao wanalinena kwa niaba Yake, mnaona, wanalitangaza. Kwa hiyo, basi, jinsi ya kumhukumu mtu huyo ni kutafuta kujua kama linatukia jinsi wanavyolisema. Halafu, likitukia, na linaendelea kutukia jinsi hiyo, vema, basi tunajua ya kwamba hilo linatoka

kwa Bwana. Ndipo sisi—ndipo tunakuwa na matumaini, basi, kujitayarisha kwa sababu jambo hilo linakuja karibuni.

20 Ninataka kusoma sehemu mbili ama tatu katika Maandiko asubuhi ya leo. Nami ninataka kusoma, kwanza, kutoka kwenye Kitabu cha Kutoka, nami ninaamini ni kama mlango wa 4 wa—wa Kutoka, kwanza kabisa.

21 Na sasa huenda nikatangaza wakati mkijiandaa kuyasoma Maandiko haya, huenda nikatangaza yale ninayotaka kuwazungumzia, kile Bwana alichoweka moyoni mwangu kuzungumzia, asubuhi ya leo. Sijui yale atakayofanya nalo, kwa watu; labda limeelekezewa mtu mmoja hapa, labda mtu fulani huko kwenye nchi ya kanda, mahali pengine. Bali ninataka kutangaza, asubuhi ya leo . . .

22 Nafikiri, Jumapili iliyopita asubuhi, nilihubiri juu ya *Shahidi Wa Kweli*. Na Jumapili hii asubuhi, Bwana akipenda, ninataka kuhubiri juu ya: *Ishara Ya Kweli Iliyopuuzwa*.

23 Ndugu Palmer alikuwa akiniambia, jana usiku, ya kwamba Jumapili iliyopita asubuhi nilizungumza juu ya somo . . . ama nilisema nitazungumza, Jumapili hii, juu ya "Njia panda nne za Kanisa." Ndipo wakati nilipoingia jana usiku . . . kwa kawaida mimi huliandika. Yale . . . Sijui kama inawabidi kufanya hivyo ama la. Bali nina mambo mengi sana, ninayojaribu kuwazia. Nikipata jambo fulani, inanibidi kuliandika kwenye kipande cha karatasi. Mnaona? Nami nilienda kuliangalia, na kile nilichokuwa nikimaanisha kwa jambo hilo hakikuwa ni njia panda nne hasa. Nililisema namna hiyo, kweli. Lakini nilichomaanisha, kilikuwa, "Namna nne za utawala wa Kanisa." Na kufanya hilo, inanibidi kukusanya historia nyingi sana pamoja. Na labda wakati huo mwingine nitakuwa nalo. Lakini inachukua wakati mwingi zaidi kidogo kuliko niliokuwa nao wakati wa kusoma, kulipata, kwa sababu inakubidi kurejea nyuma na kupata tarehe, na kadhalika.

Kwa kuwa, ninyi nyote, nyote mnafahamu ya kwamba ni kila mahali. Mbona, tunataka kuwa na hakika kabisa ya mambo haya kabla hatujayasema. Hayana budi kuwa ni ya kweli. Kwa sababu, tumesimama hapa, tukishikilia wadhifa wa juu kabisa unaoshikiliwa duniani: mhudumu. Mhudumu, na kuwa mkweli kuliko wote na wa haki, sahihi, hatuna budi kuwa hivyo. Hatuna budi kumtegemea Mungu kufanya jambo hilo.

Sasa, katika Kitabu cha Kutoka, mlango wa 4.

> *Musa akajibu akasema, . . . tazama, hawataniamini, wala hawataisikia sauti yangu: maana watasema,* B*WANA* *hakukutokea.*
>
> B*WANA* *akamwambia, Ni nini hiyo uliyo nayo mkononi* mwako? *Akasema, Ni fimbo.*

*Akamwambia, Itupe chini; akaitupa chini, nayo ikawa nyoka; Musa akakimbia mbele yake.*

*Bwana akamwambia Musa, Nyosha mkono* wako, *kamshike mkia; (akaunyosha mkono wake akamshika, naye akageuka kuwa fimbo mkononi mwake;)*

*Ili kwamba wapate kusadiki ya kwamba Bwana, Mungu wa Ibrahimu, Mungu wa Isaka, Mungu wa Yakobo, amekutokea.*

*Bwana akamwambia tena, Sasa tia mkono* wako *kifuani mwako. Akautia mkono wake kifuani mwake; naye alipoutoa, kumbe! Mkono wake ulikuwa una ukoma, umekuwa mweupe kama theluji.*

*Akasema, Tia mkono wako kifuani mwako tena. Akautia mkono wake kifuani mwake tena, na alipoutoa kifuani mwake, kumbe! Umerudia hali ya mwili wake.*

*Basi itakuwa, wasipokusadiki,* wala *kuisikiliza sauti ya ishara ya kwanza, wataisikiliza sauti ya ishara ya pili.*

Mnaona ishara hizo mbili, na kila ishara ilikuwa na sauti. Hebu nisome kifungu cha 8 tena.

*Basi itakuwa, wasipokusadiki, wala kuisikiliza sauti ya ishara ya kwanza, wataisikiliza sauti ya ishara ya pili.*

*Kisha itakuwa wasipoamini hata ishara hizo mbili, wala kuisikiliza sauti yako, basi, yatwae* maji *ya mtoni uyamwage juu ya . . . nchi kavu, na yale maji uyatwaayo mtoni yatakuwa damu juu ya nchi kavu.*

24 Na sasa katika Yohana Mtakatifu, mlango wa kwanza na kifungu cha 6, tunasoma kifungu hivi, ama kifungu hiki. Yohana Mtakatifu, mlango wa kwanza na kifungu cha 6. Na . . .

*Palikuwa na mtu, ametumwa kutoka kwa Mungu, jina lake Yohana.*

*. . . mtu aliyetumwa kutoka kwa Mungu, jina lake Yohana.*

25 Na katika Ezekieli 24:24, ninataka kuliingiza Andiko hili ndani, nikilifunga kutoka kwenye Agano la Kale, kwa manabii, kwenye Agano Jipya; kusudi mpate kuelewa ni kotekote, kuanzia Kutoka, mwanzo hadi mwisho.

*Basi ndivyo Ezekieli atakavyokuwa ishara kwenu; ninyi mtatenda sawasawa na yote aliyoyatenda yeye;* litakapokuja *jambo hili, ndipo mtakapojua ya kuwa mimi ndimi Bwana Mungu.*

Sasa hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo wakati tukimwendea kwa unyenyekevu sasa katika njia ya maombi.

26 Baba, Mungu, tunakuja katika Jina la Mungu wa Ibrahimu, Isaka, na wa Yakobo: Yesu Kristo mwenye haki. Tunakuja, tukijua ya kuwa Yeye atatusikia, kwa sababu tunakuja sio kama mtu ambaye ameingia tu jengoni, bali tunakuja kwa ujasiri pamoja na imani, tukiamini ya kwamba kile alichoahidi, hicho Yeye atakifanya. Kwa hiyo tunaomba, leo, Bwana, ya kwamba utamchukua kila mmoja wetu aliyepo, kotekote kutoka mimbarani hata nyuma ya jengo, kote katika maeneo yote, na uufungue kila moyo na utahiri kusikia kwetu, kusudi Neno la Mungu aliye hai lipate kutoka Mbinguni, asubuhi ya leo, na kumiminiwa mioyoni mwetu, ili tuweze kuamini, tunapolisikia Neno la Bwana na kama lilivyosomwa kwetu maskioni mwetu asubuhi ya leo. Nasi tunakushukuru kwa ajili ya Neno Lako. Neno Lako ndilo Kweli.

27 Na sasa, tunapouona wakati wa maovu ukikaribia, ghadhabu yote ya Mungu imelundikana angani. Na ni karibu wakati wowote ambapo jambo fulani lingeweza kutukia kwa taifa hili ambalo limekuacha, kwamba kungekuwako na mlipuko mmoja mkubwa ambao ungeliondoa taifa hili kwenye ramani ya ulimwengu, kukiweko na vitisho nyuma yake, vya nchi isiyo ya kiungu ambayo ina hamu ya kufanya hivyo. Na tukijua ya kwamba, badala ya kusongea karibu na Mungu, wanaonekana kwenda mbali zaidi. Tukijua ya kwamba Kitabu cha Ufunuo na kote katika Maandiko kimeitabiria siku hii, basi jalia tutii maonyo, Bwana, tusiwe wazembe na kushikwa na usingizi, kama ilivyokuwa. Jalia tuinuke na kujitikisa.

28 Jalia tuwe na ufahamu, leo, kuliko tulivyopata kuwa nao hapo awali. Jalia mioyo yetu na ipashwe moto sana, baada ya siku hii, hata kutakuwako na moto uliowashwa nafsini mwetu ambao utaenea kote humu nchini, Bwana, na ushuhuda ulio hai popote tulipo.

29 Wabariki wagonjwa na wanaoteseka, hao walio wahitaji, miongoni mwetu na huko nje, watu Wako, kila mahali.

30 Libariki Neno Lako, Bwana. Mtakase mtumishi Wako, na watumishi Wako wanaosikiliza, ili, pamoja, tupate kuletwa kwenye utambuzi wa karibu wa kuonekana Kwake, kuliko wakati wowote hapo kabla maishani. Sio kwamba tu ninawaombea hawa waliopo, bali wale watakaosikia kanda hii kote ulimwenguni, kwamba wapate kuingizwa kwenye Kanisa la Mungu aliye hai. Kwa kuwa tunatambua kuna njia moja tu tunayoweza kuwa mshirika wa Kanisa hili, hiyo ni kwa kuzaliwa kwa Roho, halafu tunabatizwa kwa Roho mmoja kuwa Mwili mmoja. Ninaomba, Mungu, kwa ajili ya kila mmoja wao kote ulimwenguni, kwamba Wewe ujipatie utukufu. Na jalia tuziandae nafsi zetu sana, ili kwamba kwa kilio kimoja kote ulimwenguni, tungeweza kupaza sauti, "Hata hivyo, njoo, Bwana Yesu." Tunaomba haya katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

31 *Ishara Ya Kweli Iliyopuuzwa.* Wanadamu wamezitafuta ishara, kotekote kutoka kwa Farao hata leo hii.

Naye Yesu alitwambia juu ya wa—wakati ambapo kungekuwako na watafuta ishara, na kusema ya kwamba, "Kizazi kiovu, cha zinaa kingetafuta ishara. Lakini, hata hivyo, wangepokea ishara." Nacho kizazi hicho kilikuwa kipokee ishara ya ufufuo; ambacho kingekuwa ni kizazi dhaifu, kiovu, na cha zinaa ambacho kingepewa ishara ya ufufuo.

32 Lakini kama vile Andiko hili lililo mbele zetu, katika Ezekieli mlango wa 24 na kifungu cha 24, nabii huyu alifanywa ishara. Na hiyo ndiyo ishara ninayotaka kuzungumzia.

33 Mtu huyu alifanywa ishara kwa Israeli. Na kote katika Maandiko, Mungu amewatumia manabii wake kama ishara. Nao daima wamepuuzwa. Haionekani kana kwamba wanaishika ishara hiyo. Daima wanaitafuta ishara ya mhemko.

Hata Mafarisayo wa siku za Yesu, walisema, "Utuonyeshe ishara kutoka Mbinguni."

34 Bali Yesu alirejea kwao kwamba wangeipata ishara. "Tayari mmeipata ishara." Kasema, "Mnaweza kuzitambua anga. Mnaweza kuiangalia ishara hiyo. Mnasema, 'Kama ni kwekundu, kunatanda, kesho kutakuwa na dhoruba.'"

35 Kama wangaliiangalia ishara, wangalimwangalia Yeye, na kujua kuwa Yeye alikuwa ni ishara ya Mungu kwao; kwa maana utabiri wao kumhusu Yeye ulikuwa ukitimizwa mbele ya macho yao. Lakini wangali walitafuta ishara.

36 Ni ajabu vipi kwamba watu watafanya hivyo, kwamba wataitafuta ishara wakati ishara ipo papo hapo pamoja nao, moja kwa moja miongoni mwao. Sasa, Israeli ilikuwa imefikia hali hii.

37 Na wakati mwingine mateso ambayo ishara hiyo inapaswa kupitia ni ya kushangaza sana. Mateso ambayo Yesu alipitia, apate kuithibitisha ishara ya Mungu, kwamba Yeye alikuwa ni Masihi.

38 Tunaona ya kwamba hapa, nabii huyu kijana jina lake Ezekieli daima alifanyika ishara, wakati wote. Jinsi alivyoitesa nafsi yake! Mahali pamoja hapa tunaona ambapo alilala kwa upande wake wa kushoto siku mia tatu na tisini. Mungu alimwambia achukue maharage na dengu, azichanganye, azipike, na aziweke karibu naye. Kisha aende akalalie tofali, na alale kwa ubavu wake wa kushoto, peke yake; asigeuke, kwa siku mia tatu na tisini. Wazia hilo. Kisha akasema, "Geuka kwenye ubavu wa kulia na ulale hapo siku arobaini, tena."

39 Naye akasema hapa, "Unachoona, Ezekieli," kasema, "kwa sababu unauchukua uovu wa watu, kila siku nitaihesabu kuwa ni mwaka mmoja kwa ajili yao." Ikawa, kwamba, kila siku aliyolala pale, hiyo ilimaanisha mwaka mmoja watakaokuwa

utumwani, na kwamba uovu wao ungekumbukwa kwa Mungu, Naye Mungu asingeyasikia maombi yao tena.

40 Lakini yale mateso ambayo ilimbidi mtu huyo kupitia, ni kwa nini hayo yawe ni ya lazima? Wengi wameshangaa, ni kwa nini imlazimu mtu kufanya jambo kama hilo. Ni kwa sababu watu hawatalisoma Neno, wala hawataomba. Kwa hiyo, Mungu ni mwenyezi, Naye huwapeleka manabii Wake kuwa ishara. Watu hawatasoma. Hawajali kusoma. Wala hawataomba, kwa sababu wao ni ninii sana . . . wana mambo mengine ya kufanya. Hawawezi kutenga muda wa kuomba. Nayo Biblia haiwavutii. Haina matendo mengi kwa ajili ya siku hizi za kisasa, wala siku zozote.

41 Mwajua, ninaamini ilikuwa ni Paulo aliyesema, "Ninyi ni nyaraka za Mungu, zinazosomwa na watu wote." Mungu huwatumia watu kama ishara, kuonyesha ishara Zake. Na mara nyingi ishara hiyo, na kila wakati, mara nyingi, isipokuwa iwe ni kwa watu walioteuliwa, ishara hiyo hupuuzwa na kupingwa, na kudhihakiwa, kutupiliwa mbali.

42 Na kuchukuliwa, hata katika Agano la Kale, katika siku za manabii, walichukuliwa ni watu wenye kichaa. Walidhani hao manabii walikuwa ni watu walioharibikiwa na akili, kwamba bongo lao lilikuwa na kasoro. Nao walikuwa wamewaona wakitoka nyikani na—na kufanya ishara, kisha wakarudi nyikani tena. Nao wangewadhihaki, kwa kuwa hawakuyajua Maandiko.

43 Yesu aliwaambia Mafarisayo, wakati mmoja, kuhusu ufufuo. Wao walisema, "Tulikuwa na . . . Torati inasema kwamba ndugu akifa na kumwacha mke bila—bila watoto wake, ya kwamba ndugu yake atamchukua mke huyo na kumwinulia huyo watoto, aliyekufa." Kisha kasema, "Tulikuwa na mmoja aliyekuwa na nduguze saba. Basi mmoja akamchukua mke, naye akafa, pasipo kuacha mzao. Ndipo ndugu yake akamchukua, kisha akafa; na kuendelea mpaka wa saba. Na hatimaye mwanamke huyo akafa." Kasema, "Sasa, katika ufufuo," kasema, "sasa, yeye atakuwa mke wa nani, kati ya hao saba?"

44 Loo, ninalipenda Neno hilo! Yesu alisema, "Daima mwapotea, kwa kuwa hamyajui Maandiko wala uweza wa Mungu." Loo, jinsi angaliweza kulitia hilo moto leo hii kama angalikuwa amesimama hapa! "Daima mwapotea, kwa kutoyajua Maandiko wala uweza wa Mungu." Uweza wa Mungu hushirikiana na Maandiko. "Mwapotea sana."

Ndipo akaendelea kusema, "Katika kiyama, hawaoi wala kuolewa, bali huwa kama Malaika." Hakusema wangekuwa ni Malaika, sasa, bali wangekuwa kama Malaika, tezi za jinsia zingeondolewa kwao. Hawaoi wala kuolewa.

45 Tunaishi katika siku ya maadili . . . ama siku za kibinadamu za ufalme wa kibinadamu. Lakini siku yaja ambapo kuna

Ufalme usiopatikana na mauti unaokuja, na huo Ufalme usiopatikana na mauti ndimo waliokombolewa wataishi. Hao waliokombolewa, nao wana ninii . . . Uhai unaouacha mwili huu, upate kumrudia Mungu aliyeutoa, utarudi tena kutoka kwenye ule Mti wa Uzima, siku moja, ukatawale milele.

46 Jinsi ambavyo kijana huyu, nabii huyu kijana, alivyojitolea na kuyatoa maisha yake yote kuwa ishara kwa watu wake, juu ya hukumu waliokuwa watapokea, kwa kuwa walikuwa kile ambacho tungeita "wasiojali." Hawakutaka uhusiano wowote na Mungu. Hawakuwaamini hao manabii, nao waliwadhihaki tu. Na, lakini, mbali na hayo, na haidhuru ni jinsi gani hawakutaka kuliamini, Mungu alihakikisha ya kwamba walilipata, kwa vyovyote vile.

47 Yezebeli hakutaka kukubali ya kwamba Ahabu alikuwa mchungaji wake, lakini alikuwa. Mungu alihakikisha ya kwamba aliipata hiyo ishara, hata hivyo.

Ndivyo ilivyo kwa taifa hili leo hii. Mungu mwenye haki na mkweli, kwa Neno Lake, asingeweza kuruhusu chochote, ambacho tunaona kinakaribia kutukia, pasipo kuwa na ishara mahali fulani. Amekuwa nayo daima. Sasa, hatuna budi kuitafuta. Nami nina hakika ya kwamba watu walio na ufahamu mzuri wa Maandiko wanajua jinsi ya kuangalia.

48 Nuhu alikuwa ni ishara katika siku yake, kwa watu, ya hukumu ijayo. Nuhu katika siku yake alihesabiwa kuwa ni mlokole. Alikuwa nabii. Alihesabiwa kuwa mtu asiyekuwa na akili timamu. Naye mtu huyo alipiga nyundo, mwaka baada ya mwaka, akiijenga safina, wakati hapakuwapo hata na maji duniani ila yale yaliyokuwako kwenye chemchemi. Naye akatabiri kitu ambacho kilikuwa ni cha kijinga, kwa bongo la kawaida. Akasema, "Maji yatashuka kutoka juu angani."

49 Hapana shaka, kwamba wengi wangemwambia, "Hebu nionyeshe mahali yalipo." Sayansi ingesema, "Ninaweza kuthibitisha hakuna maji kule juu."

Lakini, hata hivyo, kama Mungu alimwambia kwamba yatatokea angani, Mungu atahakikisha kwamba Neno Lake linatimia.

50 Na wakati hakukuwako na maji yaliyoonekana, wakati hakukuwahi kuwa na wingu angani, hakujawahi kunyesha hata tone moja, kamwe hakukuwako, hakukuwako na kitu kama mvua, bado, wakati wote, Nuhu alikuwa akiiandaa safina kwa ajili ya mvua. Ilikuwa ni thibitisho lililo hai ya kwamba nabii huyu aliamini yale aliyokuwa akisema, kwa kuwa alikuwa akijiandaa kwa ajili yake.

51 Na mtu yeyote ambaye kweli anaamini yale unayozungumzia, utajiandaa kwa ajili yake.

52 Hebu nisimame papa hapa, kwa dakika moja. “Kwenye siku ya Nuhu,” kama vile Yesu alivyosema, “ndivyo itakavyokuwa katika Kuja Kwake Mwana wa Adamu.” Kama makanisa, leo hii, yaliamini yale wanayozungumzia, wangetenda wasemayo.

53 Tungewezaje kuwa tunajenga sanamu kubwa za mijengo, na kutumia mamilioni ya dola kwenye mijengo, na kuyastawisha sana madhehebu na vitu kama hivyo, na kuhubiri ya kwamba Kristo yuaja wakati wowote? Tungewezaje kuendelea, na kuyaangalia makusanyiko yetu na kuyaona yakijitenga na uweza wa Mungu na kuingia katika mambo ya ulimwengu, na kuyaingiza kanisani na kuyachanganya pamoja, nasi tunaliruhusu? Kwa sababu ya kupendwa na watu, na kwa sababu ya maoni yanayopendwa na watu na tofauti za kimadhehebu, kujaribu kulishinda dhehebu hilo lingine, tungewezaje kutekeleza yale tunayohubiri? Nao walimwengu wanaona hilo. Wanajua hivyo. Kwa hiyo, dini imekuwa ni kitu kama tu kujiunga na utaratibu fulani, ama kuwa wa jumuia fulani, dini.

54 Wokovu wa Kristo sio jumuia. Sio kujiunga na kitu fulani. Ni tukio lililo hai.

55 Sasa, Nuhu alikuwa akitenda alichokuwa akizungumzia. Alisema, “Gharika la hukumu linakuja juu ya kizazi hiki dhalimu. Naye Mungu ataimwaga mvua, kutoka Mbinguni, na kuigharikisha dunia nzima.” Na si kwamba alikuwa tu akifanya hilo, bali alikuwa akiandaa njia ya kuepukia na kuwashawishi watu waingie. Bali wasingemsikiliza.

56 Lakini, Nuhu, kama nabii, alikuwa ni ishara kwa kizazi hicho, ishara ambayo ilinenwa vibaya, mtu aliyedhaniwa kuwa ni mwendawazimu; akiandaa kitu fulani, ambacho ha—hakukuwako na ushahidi mahali popote, au kamwe haukuwahi kuwepo, kwamba ingekuwa na faida yoyote.

Lakini hivyo ndivyo watu wanavyoonekana kuwazia siku hizi. Wanaweza kuwazia juu ya ngome ya mnururisho. Ngome ya mnururisho itawafaidi nini wakati hakutakuwako hata na mti ama mwamba utakaosalia duniani?

57 Tuna ngome ya mnururisho, Mkristo anayo. Kama nilivyosema, Jumapili chache zilizopita, ama nilivyowazia mahali fulani barabarani, “Sio ngome ya mnururisho. Ni ngome ya kujihami, ambamo tunaingia, kichwa kwanza, kwa moyo wetu wote, na nafsi yetu yote, na akili zetu zote, ndani ya Kristo, safina ya Mungu ya usalama.”

58 Lakini, Nuhu, mwendawazimu, alivyodhaniwa katika siku hiyo, kupitia ujinga wa kuhubiri, na kufanya ishara mbele za watu, akiwapa onyo, aliuhukumu ulimwengu. “Aliuhukumu ulimwengu, kwa kuijenga safina,” wakati hapakuwapo na maji kwake kuelea. “Aliuhukumu ulimwengu,” Biblia ilisema, Waebrania, mlango wa 11. “Aliuhukumu ulimwengu na kuiokoa

nyumba yake, kwa kujiandaa," na akiwa ishara kwa ajili ya Mungu, ya hukumu zijazo za siku hiyo. Ni jambo lenye utukufu jinsi gani!

59 Miaka ya baadaye, kulitokea ishara nyingine. Hiyo ilikuwa ni Musa, nabii. Hiyo ilikuwa ni ishara ya Mungu kwa Israeli. Walikuwa wamekuwa utumwani miaka mia nne. Ndipo Mungu akawaandalia ishara, kabla tu ya ukombozi. Naye alikuwa ni ishara ya ukombozi kwa Israeli, na ishara ya hukumu kwa Misri.

60 Nuhu alikuwa ni ishara ya ukombozi kwa watu wake, na ishara ya hukumu kwa ulimwengu uliopotea, asiyeamini. Maji yenyewe yaliyougharikisha ulimwengu na kuuzamisha ulimwengu yalikuwa ndiyo njia ya pekee ya kumwokoa Nuhu. Kitu cha pekee ambacho kingaliweza kumwokoa kilikuwa ni hiyo hukumu.

Kitu pekee kitakacholiokoa Kanisa leo hii ni hukumu, Mungu akiweka hukumu kwenye timazi.

Bali Nuhu alihubiri haidhuru. Akawa ni ishara.

61 Na sasa Israeli, baada ya miaka mia nne, walianza kulia wapate ukombozi. Naye Mungu kamwe hajifunui wala kujionyesha Mwenyewe mpaka watu Wake wamekuwa tayari kupokea kile anachoonyesha.

62 Sasa, loo, ni jambo gani lingaliweza kusemwa pale pale! Kama ninii . . . Jinsi ambavyo Mungu ameliacha taifa hili uchi. Wanajua vema zaidi. Magazeti yamelitangaza, tena na tena na tena. Ishara za Kuja Kwake zimetolewa. Nao daima wanaendelea moja kwa moja kana kwamba wanalipuuza. Hawana udhuru wowote. Tuko mwisho.

63 Mungu huwatuma tu manabii Wake wakati watu wanapomtaka nabii. Mungu huituma ishara Yake wakati watu wanapokuwa tayari kwa ajili ya ishara. Lakini, jambo ni kwamba, watu kwa nadra . . . Wanafikia mahali ambapo wanataka mhemko, ama watataka baadhi ya, "Utuonyeshe ishara kutoka Mbinguni." Bali Mungu anapoituma ishara, basi wao hawataki kuiona. "Kwa hiyo imefichwa wenye hekima na wenye akili wasiione, ipate kufunuliwa kwa watoto wachanga watakaojifunza." Wao wanaipuuza, hiyo ishara.

64 Jinsi ambavyo Israeli ilipaswa kujua, wakati yule mtoto mzuri alipozaliwa, wakati walipoangalia huko juu wakaona kwa ule—ule muda wa miaka waliyokuwa wakiishi, "Watu wako watakuwa wageni kwa muda wa miaka mia nne, katika nchi ya kigeni, lakini baadaye nitawatoa." Walipaswa kujua wakati ulikuwa umewadia, na hapo walipomwona mtoto yule mzuri amezaliwa. Huyo, hata mama na baba, Amramu na Yakobedi, hawakuogopa amri za mfalme, nao wakamweka moja kwa moja mtoni ambapo palikuwa na mamba; hakuna hata mmoja wao angalimuuma. Waliona kulikuwako na ishara, bali waliipuuza. Hawakuwa tayari kwake.

Mungu alimwingiza moja kwa moja ndani na kumweka moja kwa moja kwenye jumba la Farao, na kumwacha Farao amlee na kumpa elimu yote ambayo angeweza kupata, kuonyesha (Mungu) jinsi anavyofanya mambo, kisha akampeleka nyuma ya jangwa, akamfanya asahau yote kuhusu hiyo.

65 Farao alikuwa akimfundisha wakati huo. Mungu alikuwa akimfundisha. Farao alikuwa na miaka arobaini ya kumfundisha, ndipo Mungu akachukua miaka arobaini kumfundisha, kumfanya asahau hayo yote. Mafundisho ya mwanadamu; na mafundisho ya Mungu.

Farao alikuwa akimfundisha mwana awe kiongozi, mwanadiplomasia, awe askari wa vita, mpiganaji, apate kuwa halifa wa Farao ambaye angeidumisha Misri katika mahali pake pa juu, ikiyazamisha mataifa mengine yote na kuyafanya yamtolee Farao ushuru. Bali Mungu alimpeleka upande wa nyuma wa jangwa, akaitoa hiyo yote ndani yake. Kisha akamwonyesha, katika muda wa dakika tano, kwa kichaka kilichowaka moto, ya kwamba Yeye alikuwa ni Mungu aliye hai. Na akaondoa woga wote ndani yake; akamweka tayari. Yeye alikuwa ni ishara.

66 Mungu anataka watu Wake waombe. Na wakati Israeli walipokandamizwa sana, katika hali ambao, wasingeweza kuvumilia zaidi, wakati wao ulikuwa umefika, na mizigo yao iliongezeka kuliko walivyowazia, ndipo wakaanza kuomba. Na wakati watu wanapoanza kuomba, basi Mungu anaanza kusikia. Ulikuwa ni wakati wa Neno la Mungu kutimizwa.

67 Na kwa hiyo, wakati Amramu na Yakobedi walipoona kwamba wakati ulikuwa umewadia kwa Neno kutimizwa, waliingia katika maombi, kwa Mungu. Na kwa kawaida ni wale waombao ndio walio na mzigo, ndio wanaopata kitu. Ni wale waombao, waliokusudiwa na Mungu kufanya hivyo.

68 Tulikuwa tukizungumza asubuhi ya leo kwenye meza ya kiamshakinywa wakati tulipokuwa tukila tosti haraka na kadhalika, tupate kwenda kanisani. Kulikuwako na jambo fulani lililosemwa juu ya mtu fulani aliyekuwa, mbali na hapa, ambaye alikuwa amerejea kwenye kuvuta sigara baada ya kuponywa kansa. Nikasema, "Ni huzuni jinsi gani."

69 Kwa hiyo basi mmoja alinena akasema, "Hicho ndicho kitu kibaya kuliko vyote kuacha, kilichopo, kuvuta sigara."

70 Nikasema, "Ninajua hilo. Kwa maana, ni ibilisi." Nami nikasema, "Ni—ni ibilisi." Kisha nikasema, "Wala huwezi kuacha isipokuwa uweza wa Mungu uwe juu yako."

Ninawajua jamaa wawili katika maisha yangu ya mwanzoni, wote wawili walitaka kuwa watu wa Mungu.

Mmoja wao, mara nilipomwongoza kwa Kristo, alianza kuiwasha sigara. Alivuta pakiti tano ama sita kwa siku,

anaketi tu na kuwasha moja kwa nyingine, siku nzima. Basi akajaribu kuiwasha sigara nyingine, na kitu Fulani kisingeweza kumruhusu kufanya hivyo. Akaenda kwenye jiko, bila kujua ya kwamba Maandiko yalivihukumu vitu hivyo, akalifungua jiko na kuitupa hiyo pakiti kwenye jiko. Na hilo lilitosha.

71 Ambapo, jamaa mwingine aliyetaka kuwa Mkristo, naye akajaribu awezavyo. Akamlilia Bwana. Akaziacha, kwa majuma mawili ama matatu. Ndipo alipojirudia, katika hali hiyo, akarukwa na akili. Kisha akajirudia, akajikuta kwenye ua la nyuma, akipigapiga kipande cha bati, amerukwa na akili. Akakimbia nyumbani, upesi sana, akazinyakua sigara zake, na kuvuta pakiti nzima kabla hajaondoka nyumbani jioni hiyo, moja tu baada ya nyingine. Mnaona?

72 Mmoja aliitwa. "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu, na wote alionipa Baba watakuja Kwangu." Hilo onyo lilimaanisha nini? Ulikuwa ni Uzima, kwa mmoja. Yeye aliliona. Huwezi kuliona isipokuwa Mungu alifunue. "Limefichwa macho, wenye hekima na akili, na kufunuliwa watoto wachanga wanaoweza kujifunza." Hiyo ni kweli.

73 Amuramu na Yakobedi walijua wakati ulikuwa umewadia. Saa ilikuwa imekaribia.

74 Nami ninataka kusema hili wakati ninapolizungumzia. "Si yeye atakaye, wala yule apigaye mbio; ni Mungu ndiye arehemuye." Hiyo ni kweli. Ni Mungu.

75 Vivyo hivyo, leo hii! Loo, acheni hili lizame kilindini! Kama, leo hii, Mungu amekuita, nawe umejitenga na mambo ya ulimwengu, nao uweza wenye utukufu wa Mungu umekutakasa na mambo hayo, unapaswa kuwa mtu mwenye furaha kuliko wote ulimwenguni. Kulikuwako na mamilioni ambao wangefanya jambo hilo kama wangaliweza, bali hawawezi. Hawakukusudiwa kuupata. Hii ndiyo siku ambayo Kanisa limeitwa litoke, lijitenge. Ni tofauti, na vile ilivyokuwa. Naam.

76 Watu wanapoanza kuomba, wakati Israeli walipoanza kuomba wapate nabii, Mungu alikuwa na huyo nabii. Mungu alikuwa na huyo nabii, wakati wote, maana Mungu daima yuko hatua moja mbele zao. Alikuwa amemwandaa huyo mtu, bali Yeye alikuwa akiwangojea watu waanze kuomba, watu wawe na shauku yake.

77 Jinsi ningalisema hilo ni kama ilivyo leo hii! Tunachohitaji leo hii si mwanauamsho, sio mtu mwingine kwa dhehebu fulani kuu, ambaye atayaleta makundi yote kuunganika pamoja. Tunachohitaji leo hii ni nabii aliyetumwa kutoka kwa Mungu, akiwa na Ujumbe utakaouhukumu ulimwengu. Mungu huenda akawa na mtu huyo, kama watu wako tayari tu kwake. Mnajua yale ninayozungumzia. [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Anaye, labda, anaye mahali fulani ulimwenguni, bali inawabidi

watu kuwa na shauku yake. Mungu kamwe hayasukumii mambo kooni mwako. Inakubidi kuyataka. “Heri wenye njaa na kiu ya haki, kwa kuwa hao watashibishwa.” Hiyo ni kweli.

78 Baada ya Musa kutambuliwa . . . Baada ya watu, hasa, kujua ya kwamba walihitaji kiongozi, walianza kuomba. Walianza kumwomba Mungu awatumie kiongozi, ama mtu wa kuwatoa. Ndipo akawatumia mtu, nabii. Hiyo ilikuwa ndiyo ishara Yake. Sasa, kama mtu huyu hakuwa nabii, kama angeinuka, aseme, “Mimi ni bingwa wa kijeshi,” Israeli walikuwa na haki ya kutokumwamini mtu huyo. Kwa sababu, Mungu, katika kila wakati, pasipo kukosea, humtuma nabii. Taja wakati mmoja katika Biblia lilipotukia. Yeye daima humtuma nabii akiwa na BWANA ASEMA HIVI.

79 Hata Daudi, mwenyewe, bingwa wa jeshi aliyekuwa mkuu sana Israeli waliopata kuwa naye, na, hata hivyo, Daudi alikuwa ni nabii. Hakika, alikuwa nabii. Alikuwa ni nabii, Daudi.

80 Alikuwa akiwangojea watu wapate shauku moyoni mwao kumsikia nabii huyu ambaye alikuwa amtume.

Hakika, kulikuwako na kundi ambalo lilisema lilikuwa nayo, ambalo halikuwa nayo. Ilithibitika baadaye ya kwamba hawakuwa sahihi. Walikuwa tu wamechochewa sana, na mhemko. Nayo Biblia ilisema, “Kundi lililochangamana liliambatana nao.” Ilifanya nini? Ilisababisha shida huko nyikani. Na kila wakati, jambo la ajabu linapofanywa! Loo, laiti ningalililifanya hili lizame ndani, vizuri. Kila wakati Mungu anapotuma kitu fulani, kuna uigaji wake fidhuli, wa kimwili, unaoambatana nacho. Kila wakati, daima kitu fulani, “uigaji” wake, ambao huenenda tu vizuri na hao watu.

Bali nabii halisi wa Mungu anadumu na BWANA ASEMA HIVI. Kamwe hataondoka kwenye hayo Maandiko kama ametumwa na Mungu.

81 Musa alidumu kikamilifu kwenye Maandiko. Mungu alisema, “Nitawatoa.” Akamwambia Musa, “Nimekutuma kufanya kazi hiyo.” Naye Musa alikuwa na tukio. Alikuwa amekutana na Mungu. Alikuwa na Neno la Bwana.

82 Sababu ya Mungu kuwatuma manabii ni kwa sababu wana Neno la Bwana. Neno la Bwana huwajia manabii. Na kama hana Neno la Bwana, basi yeye si nabii.

83 Kuna uigaji mwingi sana wa kimwili unaojaribu kusema ni manabii, kotekote katika nyakati, bali daima wanaliacha Neno la Bwana. Lakini nabii wa kweli hudumu kabisa kwenye Neno. Sasa, msisahau nukuu hilo. Nabii wa kweli hudumu na BWANA ASEMA HIVI.

84 Yesu alituonya katika siku za mwisho yale yangetukia. Lakini m—mtumishi wa kweli, nabii wa kweli, kamwe hakosi kudumu na BWANA ASEMA HIVI.

85 Musa alidumu na Bwana. Yeye alikuwa ni ishara. Alikuwa ni ishara kwa Israeli ya kwamba siku yao ya ukombozi ilikuwa imekaribia, naye alikuwa ni ishara kwa Misri, ya kwamba siku ya mwisho wao ilikuwa imekaribia. Maana, walizama huko nje katika Bahari ya Chumvi, baadaye, jeshi zima la Farao. Walikuwa mwishoni mwa nguvu zao za kijeshi, naye nabii alikuwa ni ishara ya mwisho wa taifa.

86 Wazieni jambo hilo, jinsi Mungu alivyo mkuu, na ni urahisi wa jinsi gani anaofanyia kazi. Hakika, kama wasio na elimu wanaweza kuelewa hilo, walio na elimu wanapaswa kuelewa. Amina. Kama watumwa kwenye mashimo ya matope huko Misri wangeweza kufahamu ya kwamba huyo alikuwa ni nabii kutoka kwa Mungu, na ile saa ilikuwa imewadia, ni zaidi sana jinsi gani ikulu ya Farao inavyopaswa kujua. Lakini wa aina hiyo ndiyo hawafahamu hilo. Wa aina hiyo ndiyo wanaolikosa, daima. Wakati ambapo . . .

87 Musa alisimama, akiangalia kupitia madirisha hayo, hao wana wa Israeli wakipitia pale. Kwa Israeli . . . Kwa Farao, walikuwa ni watumwa na mbwa. Kwa Musa, walikuwa ni wateule wa Mungu. Biblia ilisema, ya kwamba, "Musa alichagua," akajichagulia, "kupata shutuma ya Kristo, akiihesabu ya kuwa ni utajiri mkuu kuliko anasa za dhambi, kwa kuwa aliyatazama hayo malipo." Musa alijua ya kwamba hao hawakuwa ni wakanyaga matope; hao walikuwa ni watu wenye ahadi.

88 Yeye mwenyewe, alijua kwamba alikuwa ni nani. Asingeweza kuwaambia. Hawana budi kujitambulia, wenyewe. Yeye alijua, mwenyewe, kwamba kazi Yake ilikuwa ni ipi, ku—kufanywa. Alijua ya kwamba Mungu alikuwa amemwinua kwa kusudi hili, bali asingeweza kuwaambia. Na mradi tu walikuwa ni vipofu kwake, kamwe hakujifunua waziwazi, mpaka walitambue. Ndipo, waliiona ishara hiyo, nao wakaijua.

89 Akasema, "Nitaipa Israeli ishara. Ichukue fimbo hii; ukaigeuze iwe nyoka. Hawatasikiliza hiyo. Basi tia mkono wako kifuani mwako, utoe, jiponye ukoma, ndipo wataamini. Na halafu, wasiposikia, chota maji kutoka Nile kule chini, yamwage juu ya nchi kavu, nayo maji yote yatageuka kuwa damu." Hiyo ilikuwa ni ishara ya kitaifa. Watu wataiamini. Wakati, hao walio tayari kuipokea wataiamini watakapoiona ishara ya Mungu ikitenda kazi, bali taifa halina budi kupata kitu tofauti. Kwa hiyo, akawapa wote ishara.

90 Mungu alimtumia mtu, mtu mnyenyekevu, nabii, kuwa ishara ya mwisho wa hali hiyo ya kitaifa huko chini. Mungu, tutumie mwingine. Tuinulie mwingine. Kama watu wa Mungu wangeanza kuombea jambo hilo, Yeye angemwinua. Ni, watu hawana budi kupata mzigo huo. Hawana budi kuamka. Hawana

budi kutambua. Hawana budi kujua tunaishi kwenye siku gani, na hali ya mambo yanayotuzunguka, kabla hawajapata kuamka.

Endeleeni tu kuishi jinsi mlivyopata kuishi sikuzote. “Sina budi kujenga nyumba mpya mwaka huu. Sina budi kununua gari bora kuliko la akina Joneses. Sina budi kufanya *hili*.” Loo, mengi sana ya *haya*! Unapotambua, haidhuru . . . Hilo ni sawa. Lakini huna budi kutambua, ndugu, ya kwamba vitu hivi vyote vitaangamia.

Yesu alisema, “Usimwogope yeye anayeweza kuua mwili,” bomu la atomiki la Urusi. Usimwogope yeye ambaye angeweza kuugeuza mwili huu ukawa mavumbi ya volkeno, katika dakika chache, “Bali mwogope Yeye anayeweza kuugeuza mwili namna hiyo na kuitupa nafsi kuzimuni.” Jambo ndilo hilo.

91 Kama nilivyokuwa nikizungumza na daktari, huko hospitalini wakati mama yangu alipokuwa kule. Alikuwa akizungumza kuhusu jinsi sayansi ilivyokuwa kuu, kushughulikia sehemu mbalimbali za mwili, na kuutia dawa, na kuona ni kwa nini ingeua chembe fulani, na kuokoa chembe ya uhai. Nikasema, “Ajabu hiyo. Hilo ni zuri sana.” Nikamsikiliza kwa kitambo kidogo. Lakini nikasema, “Daktari, hilo ni zuri. Ninathamini hilo. Hilo ni zuri sana. Hakika ni—ninamshukuru Mungu kwa ajili yake. Lakini, angalia, unayatumia maisha yako yote ukijaribu kupata kitu fulani katika kiumbe. Lakini kwa nini usitumie wakati fulani ukiwazia juu ya Yeye aliyekiumba, Yeye aliyekifanya, Yeye aliyekibuni? Mungu ndiye aliyekibuni.”

Muumba ni mkuu zaidi jinsi gani kuliko kiumbe alichokiumba! Ni kwa nini tunatilia mkazo sana juu ya kiumbe, wakati hatuwazii juu ya Muumba aliyeumba mbingu na nchi, na kuufanya mwili na uhai? Yeye anaweza kuuangamiza wakati wowote anaotaka, kwa sababu ni Wake.

92 Hili linakuwa jambo zuri sana, kuushughulikia mwili wa mwanadamu. Tunathamini hilo. Wanaweza kulihamisha jicho, kutoka kwa mtu mmoja hadi kwa mwingine; wachukue viungo hivyo vidogo sana, na kung’oa jicho kutoka kwenye shimo la mtu na kuliweka kwenye shimo la mtu mwingine, na mtu huyo anaweza kuona kwa jicho hilo. Hilo ni jambo zuri sana.

93 Ilikuwa kwamba, kama mama, wakati alipokuwa akienda kujifungua mtoto mchanga, na—na mtoto huyo asingeweza kuzaliwa, alikuwa—alifanywa hivyo, kwamba mtoto huyo asingeweza kuzaliwa: huyo mama na mtoto, wote wawili, walikufa. Hiyo ilikuwa sawa. Lakini ulisikia hilo kwa nadra, ilikuwa ni tofauti, labda kamwe hukusikia. Lakini siku hizi wanaweza kumchukua mama huyo baada ya yeye kuwa katika hali ya kujifungua, na kama, wakati mama amekaribia sana wa—wakati wa kujifungua, mnaona, wanaweza kumpeleka mama huyo kwenye chumba fulani na kumpa nusukaputi kidogo, na

kumtoa mtoto huyo, apate kuzaliwa kwa kawaida, wamchukue mtoto. Tunathamini hilo.

94 Niambie mfumo mmoja. Hebu funga kilango hapa nje mahali fulani, kwenye mfumo huu wa maji jijini, na uone kitakachotukia kwenye kile kilango kikuu. Yatakilipua.

Lakini, hata hivyo, tunaweza kuukata mguu, tuukate mkono, na, kwa muujiza wa Mungu, Yeye ataielekeza hiyo damu kwa njia nyingine, katika sekunde moja, na kuipitisha upesi kwa njia nyingine. Unayaokoa maisha ya huyo mtu. Ni nani anayeweza kufanya hilo? Niambie.

95 Hebu kata ateri, ikate laini kuu hapa nje mahali fulani katika maji, wakati yakisukumwa na pampu kwa kilango. Yatafanya nini? Hebu jaribu siku moja uone kitakachotukia. Hakuna njia nyingine ya kupitia. Hayana budi kulipuka yarudi kwenye kilango.

Kama Mungu hakufanya njia ya damu hii kujipitishia, mara moja, ikirudi mara moja moyoni utakufa. Kila wakati ulipokichomoa kidole chako, ingekuwa ni mauti, mara moja. Kila wakati ukikata mahali fulani, panapofungua ateri ama kitu fulani, ingekuwa ni kifo, mara moja. Kikate kidole chako, ungekufa. Hivyo tu. Ingelipusha moja kwa moja kwenye moyo wako tena. Ingekuua. Lakini Mungu . . .

96 Sasa, tunafikiri ni ajabu sana. Tunafikiri ni ajabu sana. Nasi tunashukuru jinsi sayansi imefanya, wanaweza kuzifunga hizo arteri na kuzizuia zisitoke damu. Hayo yote ni sawa. Lakini ni Nani aliyezibuni hizo? Mnaona? Tunaangalia kotekote kwenye kiumbe na kumsahau Muumba wake. Mnaona? Tunayaangalia mambo ya kawaida, na kusahau ja—jambo lote la kiroho. Hivyo ndivyo tunavyofanya.

97 Sasa, manabii wa Mungu, wao wananinii . . . wanalo Neno Lake. Hiyo ndiyo sababu watu wanawaamini.

Hiyo ndiyo sababu Mungu alimwambia Musa, alisema huko nyuma katika Mwanzo, pengi, katika Kutoka, kotekote, “Akitokea mmoja wenu, ambaye ni wa kiroho, ama, nabii, sasa tutayajuaje mambo haya?” Akasema, “Anaposema jambo fulani nalo linatimia, akisema jambo lingine, linatimia, basi mwaminini.” Mnaona? Hiyo ni ishara.

98 Kwa hiyo Yeye hutoa Neno Lake, sio kwa viongozi, sio kwa watawala wa kimabavu, bali kwa manabii. Khrushchev si ishara kwa ulimwengu. La, bwana. Hitler hakuwa ishara kwa ulimwengu. Lakini mahali fulani, pahali fulani, Mungu ana nabii mnyenyekevu akiingojea saa hii. Yeye ndiye ishara. Yeye ndiye ishara itakayouhukumu ulimwengu na kuliokoa Kanisa. Huyo nabii!

99 Eliya alikuwa ni ishara katika siku yake, nabii Eliya. Kwa ninii . . .

Yeye alikuwa—alikuwa ishara ya Neno la Mungu, hukumu kwa Misri na ukombozi kwa Israeli, kama walitaka kumwamini.

100 Hiyo siku yenye dhambi ya Eliya, wakati Israeli wote walipokuwa wamemwacha Mungu, walikuwa wamerudi katika dhambi. Walikuwa wameusahau utaratibu. Walikuwa wamesahau kuhusu kuongozwa na kutolewa na Mungu, na yule Yehova mkuu aliyeifungua Bahari ya Shamu, na kuwatoa Misri, na nabii mkuu kama Musa miongoni mwao. Walikuwa wamesahau hilo.

Tunalisahau. Ninyi Wamethodisti mnamsahau John Wesley. Ninyi Walutheri mnamsahau Martin Luther. Ninyi Wabaptisti mnamsahau John Smith. Wengi wetu tunamsahau Charles Finney, yule mkuu kuliko wote.

101 Inasemekana ya kwamba asilimia tisini na saba ya waongofu wa Finney walishikilia. Asilimia sabini na tano wa Moody walirudi nyuma katika mwaka mmoja. Nao wa Wesley, lile kundi la utakatifu, walikuwa wakirudi nyuma daima. Lakini Finney alikuwa na asilimia tisini na saba. Maskini jamaa mdogo, mwembamba, mwenye upara, alienda mimbarani na kuwaangalia wasikilizaji, namna *hiyo*, nao wanaume wangezimia, kwa maana alikaa vichakani siku moja mpaka Roho Mtakatifu akamshika. Alimshika. Alikuwa ni ishara ya mwisho, yapata miaka mia mbili iliyopita, wa ule uamsho mkuu ambao Wesley na hao wengine walikuwa nao, na hukumu ijayo.

102 Yeye alikuwa ni ishara, kizazi hicho chenye dhambi. Na jinsi Eliya angeweza kusimama pale, jasiri na mkali, peke yake, hakuna mtu aliyekuwa pamoja naye, bali yeye alikuwa ni ishara ya Mungu.

Hao makasisi wengine wote walikuwa wameenda na Ahabu, katika njia ya kisasa. Walikuwa wamekuwa wa kisasa katika kizazi hicho. Lakini jinsi maskini Ahabu, maskini Ahabu, na mafanikio yake yote makubwa, nayo yakalileta kanisa lote kwenye Ukatoli-. . . ama, sio Ukatoliki, bali ni karibu kitu kile kile: kwenye ibada za sanamu. Alikuwa amewafikisha mahali ambapo walikuwa hawana msimamo kabisa. Wengine wangeweza kuabudi *hivi*, na uhuru tu, "Mnaweza kufanya lolote mtakalo." Nao wakaingia katika hali ya namna hiyo.

103 Na jinsi ambavyo Eliya alisimama pale, jasiri, akiwa na BWANA ASEMA HIVI. Ee Mungu, tupe watu kama hao. Hakuogopa kumwambia Yezebeli kuhusu hali yake. Hakumwogopa Ahabu. Hakuogopa kwamba alikuwa ameeleweka vibaya. Yeye alisimama kwa ujasiri, na akamwendea Ahabu, na kusema, "Hata umande hautaanguka ila kwa neno langu." Amina.

104 Alikuwa ni kitu gani? Ishara kwa kizazi hicho chenye dhambi. Je! Israeli waliiona? La. Walimcheka, wakamdhihaki.

Alitabiri ya kwamba kungekuwako na ukame, ya kwamba kungekuwako—kungekuwa na shida, njaa, kufa kwa njaa. Naye alitabiri kwa ujasiri, akisimama peke yake, akiwa na BWANA ASEMA HIVI. Kasema, "Bwana, wamewaua wote walio wa kweli. Wamewaua wote. Mimi pekee ndimi mimesalia, ambaye ninasimama na Neno Lako." Shida ilihusu nini? Neno la Mungu. Eliya alitaka kudumu na Neno. Alikuwa ni nabii halisi.

105 Hao manabii wengine walikuwa wamesema, "Loo, vema, haileti tofauti kubwa. Yehova hajali, mwajua."

Yehova hujali. Haina budi kuwa ni Neno Lake. Naye Eliya alisimama kwa ujasiri juu ya Neno hilo, akiwa na BWANA ASEMA HIVI. Mungu alimpa siri ndogo, siku moja. Akasema, "Ninao elfu saba, Eliya, ambao wewe ni shahidi wao, hapa nje. Hawana ujasiri wa kutosha kutoka nje na kudai hilo. Wamejificha vichakani. Lakini, hata hivyo, moyoni mwao, hao ni watumishi Wangu. Hawajampigia Baalimu goti. Wanaogopa kufanya hivyo. Lakini, Mimi ninakupa ishara, nawe ni ishara. Simama pale, na usimame juu ya Neno Langu. Nitakushughulikia. Wape ishara." Haleluya!

Mungu, tutumie kitu kama hicho, kitakachokuwa ni ishara ya Neno la Mungu. Na kila ahadi ambayo Mungu aliahidi itathibitishwa katika mtu huyo, maana yeye ni ishara, ishara iliyosahauliwa.

106 Loo, walidhani, kwa kuwa Ahabu alikuwa ni mfalme mkuu na mataifa yote yalimwogopa, hilo lilitosha. Lakini Eliya alikuwa ni ishara ya Neno. Huyo ni nabii wa kweli, ishara ya Neno. Kwa hiyo wakati akiwa ni ishara ya Neno, hao hawakumwamini. Hawakuwa na haja naye.

107 Yeye alikuwa ishara kwa yule mjane, wakati Mungu alipomtuma mbali huko Mlima Karmeli, mbali na . . . huko kwenye kijito cha Kerithi. Akamtuma huko chini, baada ya kulishwa na kunguru, ndipo kile kijito kikakauka. Akashuka akaenda kwenye nyumba ya mjane huyu. Ni mahali pa jinsi gani kwa mhubiri kwenda! Bali alishuka akaenda kule kwa kuwa Mungu alimwambia aende. Bali alienda kule chini. Kasema, "Nimemwamuru akulishe."

108 Mjane huyo alipaswa kuwa ni ishara. Mwanamume huyo alipaswa kuwa ishara. Wakati, mjane huyo alipokuwa huko nje, alikuwa na unga wa kutosha kuoka keki moja, naye na mvulana wake waile. Na pipa la kutosha kuninii . . . Na mafuta ya kutosha katika pipa, kupika mlo mmoja mdogo, wa kuambatanisha. Akasema, "Nipo hapa nje nikiokota kuni mbili."

109 Kwenye asubuhi hiyo ya kuogofya, yenye joto, lengelenge, wakati mzee mwenye nywele za sufi, nywele zenye mvi zikining'inia mgongoni mwake, alipoenda pale, huku kichwa chake chenye upara kikimetameta, akaegemea langoni, kasema,

"Nipe maji kidogo ninywe," kisha kasema, "vile vile, niletee kipande cha mlo mkononi mwako, keki."

110 Akasema, "Sina unga wa kutosha. Niko hapa nje sasa, nikiokota kuni mbili, kumpikia mwanangu keki ndogo. Nina wa kutosha tu kupika kwa ajili yake pamoja na nafsi yangu. Tutaila kisha tufe."

111 Akasema, "Usiogope, kwa kuwa, BWANA ASEMA HIVI." Huyo ndiye mtu tunayemhitaji. Haikuwa kwamba, "Sasa, *huenda* likatukia, dada. *Huenda* likatimia. Sijui." La, la. Eliya alikuwa na msimamo chanya. "BWANA ASEMA HIVI. Lile pipa halitapunguka, wala ile chupa haitaisha, mpaka siku ile Bwana atakapoleta mvua juu ya nchi." Amina. Haya basi. Hiyo ilipaswa kuwa ni ishara ya kutosha kwake.

112 Yeye analiwakilisha kanisa leo hii. Baada ya Eliya kukaa pamoja naye kwa muda kidogo... Yeye alikuwa na mvulana mdogo. Akashikwa na ugonjwa. Ugonjwa wake ulikuwa mbaya sana hata haikusalia pumzi ndani yake. Akafa. Ndipo yeye alifanya nini? Kanisa limekwisha kuona ishara hizo. Lakini, ni nini, mara maafa madogo yakiingia, upesi anataka kulilaumu kanisa kwa ajili yake. Alitaka kumlaumu Eliya. Alisema, "Ewe mtu wa Mungu, sasa umekuja hapa ili kunikumbusha dhambi zangu na kuutwaa uhai wa mwanangu."

113 Eliya akamchukua huyo mwana, akapanda orofani alimokuwa akilala kule juu, akamlaza kwenye kitanda chake mwenyewe, akajinyosha juu yake, kasema, "Bwana Mungu," Haleluya, "irudishe nafsi ya mvulana huyu." Ndipo huyo mtoto mchanga akaamka.

114 Akamrudisha chini. Mwanamke huyo akamwangalia huyo mtoto mchanga, kisha akamwangalia yeye, ndipo akajua kitu fulani kilikuwako pale. Akasema, "Kwa jambo hili ninajua ya kwamba Neno la Mungu limo kinywani mwako." Amina. Yeye alikuwa ni ishara kwa mjane huyo. Wakati alipoziona nguvu za Mungu, ambaye hufanya hai ama anaweza kuua, akimfufua mtoto wake mchanga aliyekuwa amekufa, yeye alisema, "Kwa jambo hili ninajua kwamba wewe ni mtu wa Mungu." Alijua hilo.

Mataifa siku hizi wangelicheka jambo hilo, kama walivyofanya wakati huo. Wasingeliamini. Lakini mwanamke huyo alijua vinginevyo. Ilikuwa ni ishara wakati huo, kama vile yeye alivyokuwa ni ishara, kumfufua mtoto wake aliyekuwa amekufa awe hai tena. Hao manabii daima ni ishara za Mungu.

115 Wakati Eliya basi alipoagiza shindano la kuamua, alisema, "Kama Mungu ni Mungu, mtumikieni. Kama Baali ni mungu, mtumikieni."

Hiyo si ingekuwa ni siku ya kushangaza ya Eliya leo hii? Kama siasa ndiyo mungu, itumikieni. Tuna nini katika siasa? Tumefanya nini? Hatuna kitu ila lundo la uozo. Hatuna kitu.

Lakini tumepoteza kila, karibu kila rafiki tuliye naye, kupitia kwa mataifa. Hapa, juma lililopita, tuliyapoteza mataifa mawili ama matatu zaidi kwa ukomunisti. Tunawatoza watu kodi na kuzichukua fedha zao, na kuzituma huko kuwalisha watu hao wanaogeuka wakaingia ukomunisti mara wanapoimarika. Ni unafiki. Hiyo ni kweli.

116 Tunakiri kuwa tu Wakristo. Hebu na tuwe kama Wakristo, basi, sio kwa kuwalisha vitu kama hivyo. Hiyo haina uhusiano wowote na—na . . . Mtu wa kawaida mwenye moyo safi atafanya hivyo. Hiyo ni dini. Huo sio wokovu.

Watu wengi sana huichanganya dini na wokovu. Dini ni kuwalisha wajane na maskini, na kadhalika. Hiyo ni dini. Lakini wokovu ni Kuzaliwa upya, kuzaliwa mara ya pili. Hiyo ni tofauti. Dini, Uislamu ni dini. Zipo dini nyingi.

117 Sasa, juu ya Mlima Karmeli, siku ile alipoagiza shindano la kuamua, naye akamwita Ahabu na maelfu ya makuhani waliokuwa wa hekalu la madhehebu yao. Yeye aliwaita juu ya Mlima Karmeli, kasema, "Pandeni mje huku juu. Tukutane huku juu. Nitakabiliana na kundi hilo lote." Yeye alifanya nini? Alikuwa na BWANA ASEMA HIVI. Hakuogopa. Alisema, "Toeni fahali dhabihu. Mkamwite Baalimu. Mungu yule ajibuye kwa moto na awe ndiye Mungu."

118 Kwa hiyo, siku nzima, mpaka . . . tangu asubuhi mpaka baada ya chakula cha jioni, walirukaruka madhabahuni. Walijikatakata kwa visu. Wakapiga makelele. Wakapiga mayowe. Eliya alitembea huku na huku, kasema, "Pigeni mayowe zaidi. Huenda ikawa ameenda kwenye ziara ya kuvua samaki, ama chochote kile. Yuko nje anawinda, ama chochote kile."

Kwa kuwa, yeye alikuwa na BWANA ASEMA HIVI. Aliridhika. Alikuwa na Neno la Mungu.

Ndugu, dada, mtu anahitaji nini zaidi ya ahadi ya Mungu? Mungu alisema angefanya jambo hilo. Ni Ibrahimu. Alimhesabu Mungu kuwa anaweza kufanya alilosema. Alijua kwamba Mungu angeweza kulifanya, kwa kuwa Mungu alisema hivyo.

119 Kwa hiyo yeye—kwa hiyo akawaita wapande kule juu. Na kwa hiyo wakajikatakata kwa visu wenyewe, na kupiga mayowe na kupaza sauti siku nzima, hata kwenye dhabihu ya jioni. Ndipo, Eliya, angalieni jinsi alivyofanya jambo hilo. Jambo la kwanza alilofanya lilikuwa ni kuyafingirisha mawe kumi na mawili pamoja.

Mungu hajagawanyika. Madhehebu ndiyo yanayoyagawanya makanisa, bali si Mungu.

Mtu alisema, "Je! wewe ni Mkristo?"

120 "Mimi ni Mbaptisti." Kwa hiyo hiyo si zaidi ya kusema yeye ni nguruwe.

121 Wasema, "Mimi ni Mmethodisti." Vema, hiyo si zaidi ya nguruwe, tena, kwa Mungu.

122 Nasema, "Je! wewe ni Mkristo?" Kuwa Mkristo, huna budi kuwa kama Kristo, Mungu amefanya maskani ndani yako, pamoja na Roho Mtakatifu, kama alivyoshuka kwenye Siku ya Pentekoste. Sio mhemko fulani, bali ninamaanisha pentekoste halisi. Mnaona? Kweli.

123 "Mimi ni Mpentekoste. Mimi ni wa Umoja. Mimi—mimi ni wa utatu. Mimi . . . " Loo, jamani! Hiyo si zaidi ya kusema ulikuwa kitu kingine. Halimaanishi kitu kwa Mungu. Hilo hugawanya.

124 Hilo ndilo lililokuwa limetukia kule chini miongoni mwa hao makasisi. Lakini Eliya aliyafingirisha mawe haya kumi na mawili pamoja, kuonyesha ya kwamba Mungu ni Mungu mmoja juu ya wote. Akayafingirisha pamoja.

125 Kwa hiyo, wakati alipoyakusanya pamoja namna hiyo, yeye alimwua fahali mdogo na kumweka juu ya madhabahu, juu ya kuni. Akasema, "Sasa, ili kuhakikisha hakuna uigaji katika jambo hili, nendeni mkanichotee mitungi kumi na miwili ya maji." Na kwa kweli akaziloweshа kuni hizo kwa maji. Loo, haleluya! Alitaka kuonyesha ya kwamba Mungu alikuwa ni Mungu. Kwa sababu, kwa nini? Yeye alikuwa na BWANA ASEMA HIVI. Alikuwa ni nabii. Alikuwa na Neno la Mungu.

126 Kwa hiyo, siku hiyo, kama wakisema watakufukuza kanisani, watafanya *hili*, lile *lingine*, kama umebatizwa katika Jina la Yesu, na mambo haya yote mbalimbali namna hiyo: upuuzi. Ni BWANA ASEMA HIVI.

127 Mtu wa kupendeza, hivi majuzi usiku, aliongea nami, wakaja wakanikumbatia, na kusema, "Ndugu Branham," kasema, "ninataka kukuuliza jambo fulani." Kasema, "Kama tu ungeweza kupatana kidogo, kitu hiki unachozungumzia."

Nikasema, "Kitu gani?"

Kasema, "Ubatizo huu wote." Kasema, "Makanisa ya Chikago na yote huku yanakutaka sana, bali wanahofia utautaja huo."

128 Nikasema, "Hakika, nitautaja. Bila shaka, nitautaja."

Kasema, "Vema, hilo ndilo jambo pekee walilo nalo dhidi yako."

129 Nikasema, "Basi hawanipingi mimi. Si mimi niliyesema hilo. Mungu alilisema. Ninampa changamoto yeyote wa hao aje na kuthibitisha si sahihi." Mnaona?

130 Kasema, "Vema, unaona, u—unapaswa kukubali na kufanya ushirika."

Hilo ni jambo lile lile walilomtaka yeye kufanya. Mungu hapatani. La, bwana. Yeye hapatani.

Yeye alisema—alisema, "Sasa, Ndugu Branham, ninataka kukuuliza jambo fulani. Je! Malaika wa Bwana. . . " Kasema, "Sote tunamwamini Malaika wa Bwana. Je! Malaika wa Bwana alikwambia Hili?"

131 Nikasema, "Sijali yale Malaika wa Bwana angesema. Kama Yeye, Malaika wa Bwana, Yeye atasema *Hivyo*. Lakini kama angalisema kitu kingine tofauti, Yeye hakuwa ni Malaika wa Bwana." Nikasema, "Haidhuru yale Malaika, ama chochote kile kilichosema, Paulo alisema, 'Ingawa Malaika kutoka Mbinguni atawahubiri Injili nyingine yoyote, na alaaniwe.'"

132 Malaika na kila mtu, kitu fulani cha kimwili chenye kiburi, kinasema kuhusu Malaika. Joseph Smith, Brigham Young, na madhehebu yote mbalimbali, ya Wasabato na chochote kile, wanaona kila namna ya mambo kama hayo, bali daima ni kinyume na Neno.

133 Lakini, Mungu hulitetea Neno Lake. Ni Neno Lake. Nilisema, "Ni Neno la Bwana. Hakika. Yote niliyopata kujua nilifundishwa Naye. Kamwe sikwenda kwenye seminari wala shule. Linatoka Kwake." Nikasema, "Kama lilikuwa ni kinyume. . .Kama lingalikuwa ni kinyume na Hilo, nisingemwamini. Maana, hilo ni Neno la Mungu, ni la kwanza. Kingine chochote kitakuwa ni uongo." Neno la Mungu, dumuni Nalo.

134 Kwa hiyo, Eliya, wakati alipomaliza, aliyalowesha magogo hayo kabisa kwa maji, kwa mitungu kumi na miwili ya maji. Akayamwaga huko juu. Akajitokeza pale, mtulivu tu awezavyo. Kwa nini? Mungu hawezi kusema uongo. Mungu alimwambia. Yeye alisema, "Bwana Mungu wa Ibrahimu, Isaka, na wa Israeli, na ijulikane leo hii ya kwamba Wewe ni Mungu, nami ni mtumishi Wako. Nami nimefanya jambo hili kwa amri Yako, kwa kuwa ni BWANA ASEMA HIVI. Nilifanya hili kwa sababu uliniambia nilifanye, kwa kuwa ni kulingana na Neno Lako. Na ijulikane sasa kwamba Wewe ni Mungu."

Ndipo Moto wa Mungu ukashuka, ukaiteketeza dhabihu, magogo yaliyolowa maji, ukaiteketeza miamba, na chochote kile, na kuondolea mbali kila kitu. Ndipo Israeli wakalia, wale elfu saba, "Mungu na awe ni Mungu."

135 Eliya, ni vizuri jinsi gani kuuona maskini mwili huo mdogo, ulioonekana dhaifu, uliokonda na kujaa makunyanzi, maskini fimbo ile ndogo mkononi mwake, pipa dogo la mafuta likining'inia ubavuni mwake, amejizungushia kipande cha ngozi ya kondoo. Mbona, wangemtia gerezani leo hii kama angalitembea barabarani; bali wanawaacha wanawake wavae kaptura; bali hakika wasingefanya hilo, mnaona, namna hiyo, kutoka. Kwa hiyo, basi, bali hawa hapa wanakuja. Hawa hapa wanashuka wakija, kupitia pale, kuvuka kilima, kwenye fimbo hii.

136 Sasa, Mlima Karmeli si maskini—maskini sehemu ndogo tupu iliyoko katikati ya jangwa. Ni mlima mkubwa. Unaenea, kwa namna fulani unakaa kipembe namna *hii*, na unaenda hadi kwenye kilele, nao unaiangalia bahari. Naye Eliya na Gehazi wakapanda upesi mpaka juu, kileleni. Ndipo Eliya akainamisha uso wake chini pale, akaanza kumlilia Mungu, huku mgongo wake umeelekezwa magharibi, kuelekea jua. Miaka mitatu na miezi sita, hata umande haukuwa umeanguka. Akamwambia Gehazi, "Nenda ukaangalie uone kama unaona chochote, wingu huko juu ya bahari."

Akasimama juu ya mlima huu, akiangalia *huko*, kasema, "Sioni chochote."

137 Akakaa pale pale. "Mungu, ikiwa watu hawa wametubu, ikiwa watu hawa wamekurudia Wewe, ikiwa wako tayari kuuondokea upuuzi huu wote na kulirudia Neno Lako, basi Wewe ni Mungu, kulijibu Neno Lako."

138 Hebu niseme jambo lile lile leo hii. Hebu yachukueni madhehebu haya na kuyavunjilia mbali, msahau tofauti hizi za kimadhehebu, na muwaache watu walirudie Neno la Mungu, kwenye mstari wa kuchongwa. Nitawathibitishia ya kwamba kuna Mungu ambaye angali anaweza kujibu kwa Moto.

139 Hebu watu na wamwite Mungu. Hebu. . .?. . .wamwitie mtu. Hebu watu wamwitie nabii. Mungu atamleta jukwaani. Ninayapa mataifa changamoto yafanye hivyo. Inamisheni nyuso zenu mkamlilie Mungu, amtume mkombozi, ndipo mwone litakalotukia. Hebu fanyeni hivyo wakati mmoja, Mungu atajibu. Mungu daima hujibu.

140 Akainama chini na kusema, "Mungu, na iwe leo hii. Watu hawa wakati mmoja walikukataa. Watu hawa wamegawanyika katika kila namna ya madhehebu huko nje. Lakini, leo, Wewe umejithibitisha. Wewe ni Mungu. Nao watu wakasema, 'Mtupilieni mbali Baalimu.' Nami nimewaua hao maelfu ya makuhani. Hawako tena sasa, Bwana. Pingamizi zote zimekwisha, maskini vizuizi vilivyotutenganisha."

Mmethodisti angetaka kuja kuabudu pamoja na Mbaptisti; Mbaptisti angetaka kuja pamoja na Wapentekoste; wenye moyo mweupe kule chini, wale elfu saba waaminifu. Bali hawawezi kufanya hivyo. Kama wakifanya, wanafukuzwa makanisani. Baadhi yao hawajali. Wanakuja, hata hivyo. Hiyo ni kweli.

141 Lakini wajalie wote wavunjilie mbali chuki hizo na waungane pamoja, na kusema, "Tutasahau kanuni hizi zote hapa za imani na katekisimo, na kila kitu tunachosoma. Jalia tulirudie Neno la Bwana." Angalieni kitakachotukia basi. Mungu atawainulia nabii, hakika atawainulia, ambaye atawashushia Hilo moja kwa moja, ikiwa wako tayari kulipokea. Kwanza, hawana budi kuomba. Mungu huwa anangoja.

142 Si ni ajabu ya kwamba Mungu anawataka watu wahusike katika hilo? Wakati Yesu alipoyatazama mavuno, Yeye alisema, “Mavuno yako tayari. Wafanya kazi ni wachache. Mwombeni Bwana wa mavuno,” huyo alikuwa ni Yeye. “Niombeni Mimi, kwamba nitawatuma wafanya kazi kwenye mavuno Yangu.” Kuna sehemu unayopaswa kutumikia. Mungu analingojea Kanisa Lake limwite. Daima amefanya hivyo. Mungu leo hii anawangojea watu wamwite mtumishi Wake kazini. Naye huyo mtumishi hawezi kuingia kazini mpaka watu waombe.

143 Israeli wasingeweza kuingia kazini huko chini, kwa ishara na maajabu, mpaka walipoinamisha uso wao na kuomba wapate mkombozi. Mungu alikuwa na mkombozi Wake. Mungu alikuwa na nabii amekaa huko nyikani, akamweka huko kwa muda wa miaka arobaini, akiwangojea wajiweke sawa, waombe. Lakini walipojiweka sawa na kuanza kuomba, basi Mungu alimtuma mkombozi.

Mungu atafanya jambo lilo hilo leo hii, kama watu wangekusanyika tu pamoja, waanze kuomba. Vema.

144 Yeye alikuwa ni ishara kwa hao manabii wa uongo na kwa Ahabu, ya kwamba yeye alikuwa ni mtumishi wa Mungu. Alikuwa ni nabii wa Mungu. Ndipo, yeye pia alikuwa ni ishara kwa Israeli, kwamba angeweza kuzifunga mbingu ama kuzifungua mbingu, wakati alipotaka. Hakika alikuwa nabii.

Niambie mtu anayeweza kuzifunga mbingu, nionyeshe mmoja anayeweza kuzifungua mbingu, nje ya Mungu. Nalo Neno la, Mungu, Neno la Mungu liko pamoja na manabii.

145 Mikaya, ishara kwa Yehoshafati. Mikaya alikuwa ni ishara kwa Yehoshafati, ya kwamba Mungu humweka nabii wa kweli tayari.

146 Sasa angalieni. Alikuwa na manabii mia nne, Ahabu alikuwa nao, naye akawaita hao manabii mia nne. Nao kwa nia moja wakamwambia. Na hata hivyo, ndani ya moyo huo wa Yehoshafati, mtu wa Mungu, yeye alijua kulikuwa na kasoro fulani. Alijua kulikuwa na kasoro fulani. Akasema, “Hivi huna mmoja zaidi?”

147 “Baada ya mia nne waliosimama pale?” Akasema, “Hawa wote ni manabii, manabii wa Yehova.” Kuna—kuna Wamethodisti, Wabaptisti, Wapresbiteri, Wa Umoja, loo, jamani, jamani, wa utatu, na wa kila namna. “Tunao wote hapa, na kwa nia moja wanasema hili ndilo taifa kuu sana lililopo. Hatuna cha kutuogofya.” Kama vile mvulana mdogo anayepiga mbinja makaburini, mnajua, wakati anaogopa. Msijali juu ya hilo.

Kasema, “Lakini hivi huna mmoja zaidi?”

Kasema, “Loo, naam, yupo mwingine hapa, lakini,” kasema, “namchukia.” Mnaona? Kasema, “Yeye daima anainenea mabaya nchi hii. Daima anasema jambo baya litatupata sisi.”

148 Yehoshafati akasema, "Ninge—ningetaka kumsikia." Loo, naam!

Yeye alikuwa ni nini? Ishara. Haidhuru ni mashirika mangapi au madhehebu, Mungu angali anaye nabii anayedumu na Neno.

149 Yehoshafati alijua ya kwamba Ahabu alikuwa amekusudiwa maangamizi, kwa kuwa yule nabii halisi, Eliya, alikuwa ni ishara kwa mataifa, kasema, "Mbwa watairamba damu yako, kwa ajili ya kuja hapa." Hiyo ni kweli. Alijua ya kwamba yeye pamoja na Yezebeli watapatwa na hayo. Alijua hivyo. Mnaona?

150 Naye Mikaya, Mikaya akasema. Walimjia na kusema, "Sasa, nitakwambia, kama unataka kujiunga na shirika lingine, nitakwambia utakachofanya. Wewe kubali tu ya kwamba wahubiri hawa wote wanasema kweli. Unaona? Wewe mwambie, 'Kwea.'" Ndipo kasema, "Wewe kubali tu." Kasema, "Nitakwambia kile tutakachofanya. Tutafanya . . . Tutahakikisha ya kwamba wewe utaingia kwenye shirika letu, kama utafanya tu hivyo, unaona, kama utapatana tu kwenye machache ya mambo haya hapa ambayo unasema habari zake. Wewe onyesha tu, nenda, kubaliana nao, ambatana nao." A—ha! Ungeweza kuwazia nabii wa kweli wa Mungu akiliacha Neno la Mungu? Ungeweza?

"Vema," jamaa hawa walisema, "lakini, tuliona ono," hawa manabii mia nne. "Tunajua. Sisi ni manabii. Tunajua, kwa kuwa sisi ni manabii."

151 Mikaya akasema, "Sina shaka ila kwamba mliona ono. Silitilii shaka hata kidogo, lile mliloona, ono, bali halilingani na lile Neno." Amina. Kasema, "Niliona ono, pia." Amina. Loo, rehema! Yeye alikuwa ni ishara. Alikuwa ni ishara. Akasema, "Niliona ono, nami nikawaona Israeli, kama kondoo, waliotawanyika kilimani, bila mchungaji."

Naye huyu kiongozi mkuu, askofu, akaenda pale na kumpiga kofi mdomoni. Kasema, "Roho wa Mungu alienda wapi wakati alipotoka kwangu?"

152 Akasema, "Utaona wakati ukiwa gerezani. Utaona."

Yeye, Ahabu akasema, "Mweke jamaa huyo gerezani. Mlishe mkate huu wa huzuni, na umpe maji ya huzuni, anywe." Kasema, "Nitakaporudi katika amani," kasema, "basi nitamshughulikia."

153 Maskini Mikaya akasimama pale akiwa na BWANA ASEMA HIVI. Akasema, "Ukirudi kamwe, Mungu hakunizungumzia." A-ha! Jambo ndilo hilo. Alikuwa ni kitu gani? Alikuwa ni ishara, ya kwamba manabii wa Yehova, manabii wa Mungu, hudumu na Neno la Mungu.

154 Mkiwa na nabii anayesema inakupasa kubatizwa katika sifa za "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu," ni nabii wa uongo.

Mkisema kuna nabii miongoni mwenu, anayesema, "Kuna Miungu watatu," ni nabii wa uongo. Hakuna Maandiko ya lolote la hayo. Hiyo ni kweli. Bali nabii wa kweli wa Mungu atadumu na Neno hilo. Na endapo ono lake ni kinyume na Neno hilo, yeye si nabii wa kweli aliyetoka kwa Mungu.

155 Hakuna mahali popote, katika Biblia, mtu yeyote alipata kubatizwa katika sifa za "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu."

156 Mwangalieni Paulo, huko juu gerezani, maskini Myahudi mdogo, mwenye pua iliyopinda, mwenye upara, amelala pale juu, akitumia miaka ishirini, jela la Kirumi. Yeye aliandika nyaraka hizi. Sasa, unafikiri wanawake wahubiri waliwazia nini juu ya Paulo, wakati aliposema, "Wanawake na wanyamaze makanisani. Siwaruhusu kuzungumza"? Ninawazia hao wangalimshambulia kwelikweki.

Unafikiri hao maaskofu waliwazia nini, hao maaskofu, waliposema mambo haya yote mbalimbali? "Achaneni na upuuzi *huu* hapa, na *huu* hapa, na wote *huu*, *ule*? Ati Paulo? Niambieni, jamaa huyu ni nani, hata hivyo, jamaa huyu anayekaa pale gerezani?" Lakini alikuwa amekutana na Yesu. Alijua kile alichokuwa akizungumzia.

Na kutokana na kundi lilo hilo, baada ya kifo cha Paulo, hatimaye waliunda, kutoka kwenye kundi hilo la maaskofu na watu wakuu, hadi kwenye Baraza la Nikea, na hilo likaanzisha kanisa Katoliki, wakiliacha Neno la Mungu. Hapo ukaja ule wenu wa "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu." Ninampa changamoto mtu yeyote, mahali popote, taifa lolote, kukanusha hilo.

157 BWANA ASEMA HIVI. Ubatizo wa kutumia sifa za "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu" ni wa uongo. BWANA ASEMA HIVI. Ninamwamuru kila mmoja wenu, hapa ama kwenye kanda, ambaye hajabatizwa katika Jina la "Yesu Kristo," abatizwe tena katika Jina la Yesu Kristo.

158 Paulo, katika Matendo, 5:9, ama, 19:5, alisema, "Je! mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?"

Wakasema, "Hatujui kama kuna Roho Mtakatifu yeyote."

Kasema, "Basi mlibatizwaje?"

159 Wakasema, "Tumebatizwa," bali sio katika ubatizo wa Kikristo.

"Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu" sio ubatizo wa Kikristo. Hakuna Mkristo aliyepata kubatizwa namna hiyo, katika Biblia ama kwa mamia ya miaka baada ya Biblia. Ni kanuni ya imani ya Katoliki, wala si Fundisho la Kikristo. Nionyesheni katika Biblia. Ni—ni ulaghai. Ni kazi ya mashetani.

Simaanishi kusema ya kwamba watu waliobatizwa jinsi hiyo wako hivyo. Mungu anao watu wengi huko nje leo hii wasiojua vema zaidi.

160 Lakini, wakati umewadia, hatuna budi kurudi kwenye Neno kama tunamtarajia Mungu kutenda kazi siku hii kama alivyotenda wakati huo.

161 Nilimwambia mama yangu wakati alipokuwa akifa, kabla hajafa. Nikasema, "Mama, nilipokuwa Mkristo, kama mvulana, nilianza kutafuta na kutaka kujua. Nilijua kulikuwako na Mungu, kutokana na maono unayoyajua, na mambo yaliyotukia kote katika maisha." Nikasema, "Ndipo nikakuta kanisa Katoliki lilisema, 'Sisi ndio kanisa. Haileti tofauti yoyote yale Biblia inayosema. Tunaamini Hilo kwamba ni kweli, bali, sisi ndio kanisa. Tusemayo, Mungu huyafunga Mbinguni.' Na kwa hiyo, basi, hao huufanya *hivi*. Hilo ni kundi moja. Walutheri walisema, 'Wamekosea. Tunaliamini namna *hii*.' Wabaptisti wanasema, 'Wote wamekosea. Tunaliamini *hivi*.' Na kuna mamia ya makundi hayo."

Mbona, ungewezaje kamwe kuwa na imani? Ni gani kati yayo lililo sahihi? Kuna Jambo moja lililo sahihi. Sikulijua wakati huo.

162 Nikasema, "Mama, nilirudi kwenye Biblia nikapata jinsi hao mitume wa mwanzoni, aina ya kanisa walilokuwa nalo, jinsi walivyofundisha, na mambo waliyofanya. Nililifanya jinsi hasa walivyofanya, jinsi Biblia ilivyosema, nami nikapata matokeo yale yale." Amina. Samahani tamshi hili, bali thi—thibitisho la mlo ni kwenye kuula. Hiyo ni kweli. Nilipata matokeo yale yale waliyopata. Naam.

163 Kwa hiyo, huwezi kujenga matumaini juu ya kitu ambacho kina njia mia tisa mbalimbali, za kwenda *huku* na kwenda *kule*.

Ndipo nikakuta, huko kwenye Biblia, kwamba Yesu alisema, Mwenyewe, "Kama mtu yeyote atatoa Neno moja, ama kulibadilisha, katika Kitabu hiki; mtu yeyote atakayeongeza chochote Kwake, ama kutoa chochote kutoka Kwake; huyo ataondolewa, sehemu yake katika Kitabu cha Uzima." Inaonyesha jina lake lilikuwa mle ndani, vema, bali litaondolewa. Loo!

164 Hatuna budi kurudi kwenye Neno hili. "Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitashindwa kamwe." Naam, bwana. "Neno la kila mtu na liwe uongo. Langu liwe kweli," kasema Yesu. Na tudumu na Neno. Naam. Loo, jamani! Naam.

165 Yehoshafati anajua ya kwamba Mungu huwa na nabii halisi, wa kweli anayedumu na Neno Lake wala hatapatana Nalo. La, bwana.

166 Yeye alidumu moja kwa moja Nalo. Mia nne wakimpinga, pamoja na unabii wao, pia. Bali lake lilikuwa ni Neno la Mungu, likiwa na ishara ile ile na kadhalika.

Nami nasema, leo hii, kile tunachohitaji leo hii ni mwanamume, nabii, ainuke miongoni mwetu, ambaye atadumu

na Neno la Mungu haidhuru mtu yeyote mwingine anasema nini, ama chochote dhehebu lililosema.

167 Mikaya hakuwa na ushirikiano. Musa hakuwa na ushirikiano. Nuhu hakuwa na ushirikiano. Hakuna mmoja wao, hata, aliye na ushirikiano. Wote wanawapinga. Lakini hao ni ishara katika siku ovu kabla ya Mungu kutuma hukumu. Naye Mungu hutimiza Neno Lake na anataka Neno Lake lidumishwe na watu Wake. Bwana asifiwe.

Sasa, tukifikia kwenye kufunga, kwa dakika chache tu sasa. Sasa sikilizeni kwa makini.

168 "Kulikuwako na mtu aliyetumwa kutoka kwa Mungu jina lake Yohana," ishara ya nabii. Kabla Yesu hajapata kuja duniani, kujitangaza Mwenyewe, Yeye alimtuma nabii mbele Zake. Alifanya hivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Yeye alimtuma nabii, yule Eliya wa Agano la Kale, alitabiriwa kuja katika uweza wa Eliya wa Agano la Kale. Alikuwa awe ni ishara ya nabii kwamba Yesu yuaja, kwamba kulipaswa kuwa na Masihi atakayekuja.

169 Naye Yohana alitoka nyikani, alikuwa ni ishara ya kwamba Masihi alikuwa njiani. Wakati Yohana alipotokea, Israeli walipaswa kujua, kwa manabii wao.

Hapo ndipo watu wanapolikosa. Hawaamini manabii wao. Hawaamini. "Hatuamini yale Petro alisema yalikuwa ni kweli, kwenye Siku ya Pentekoste." Hawaamini hiyo ni kweli. Hawaamini yale Paulo aliyosema, jambo lile lile ambalo Petro alifanya. Kasema, "Ikiwa Malaika kutoka Mbinguni atahubiri neno lingine lolote, na alaaniwe." Hawaamini hilo. Mnaona? Hawaliamini.

Nao hawakuwaamini manabii wao. Kama wangalijua, wangalijua ya kwamba Isaya alisema, "Kutakuwako na sauti ya mtu aliaye nyikani, ambayo itatengeneza njia mbele za Bwana." Iliwapasa kujua hilo. Yeye alikuwa ni nabii, mkuu wa manabii. Yeye aliwaambia, bali hawakuamini. La, la. Yeye alisema, "Yuaja Masihi."

170 Mtu huyu alikuwa ni mtu aliyetumwa kutoka kwa Mungu. Loo, ndugu! Hakuwa na wafuasi wowote. Mungu alimpa wafuasi, kundi dogo, kama tu alivyomfanyia Eliya. Mungu alimpa wafuasi wake. Hakuwapata kutoka kwenye shirika fulani la kisiasa. Yeye alilihubiri Neno, akadumu kwenye Neno la Mungu, ndipo Mungu akampa kundi dogo. Eliya alidumu kwenye Neno la Mungu. Mungu akampa kundi dogo.

171 Mtu huyu hakuwa na ushirikiano. Hakuwa na wafuasi, hakuwa na ushirikiano, hakuwa mfuasi wa dhehebu lolote, hakuomba kitu chochote wala hakuogopa chochote. Huyo alikuwa ni Yohana. Kwa nini? Yeye alikuwa ni mtu aliyetumwa kutoka kwa Mungu. Hiyo ndiyo sababu alisimama. Yeye alikuwa ni Eliya akisimama pale, kuwathibitishia watu ya kwamba

Masihi alikuwa yuaja. Alisema, "Mimi ni sauti ya mtu aliaye nyikani, kama asemavyo nabii Isaya. Iweni tayari kukutana na Bwana."

172 Hao Mafarisayo na Masadukayo walisimama huko nje na kubishana kuhusu makoti yao na kadhalika. Mara walipokuwa wakibishana na kuzozana kuhusu hilo, moja kwa moja katikati yao akaja Masihi, akitembea.

173 Yohana akasema, "Tazameni, yule pale." Haleluya! Mwangalieni. Alikuwa amemtambulisha. "Yule pale. Yeye anasimama moja kwa moja miongoni mwenu sasa."

Yapata wakati huo, mbingu zikanguruma. Yesu akaingia majini. Ndipo Yohana akashuhudia, akimwona Roho wa Mungu, kama hua, akishuka. Sauti ikilia, "Huyu ni Mwanangu nimpendaye ambaye ninapendezwa kukaa ndani Yake." Lo, jamani, jamani!

174 Yohana akasema, "Sasa sina budi kupungua. Yeye ataongezeka." Loo, ni nabii wa jinsi gani, ishara kwa Israeli! Naam, bwana.

175 Yeye alikuwa ni mtu aliyetumwa kutoka kwa Mungu, ingawa baba yake alikuwa ni kuhani. Loo, naam. Baba yake, Zekaria, alikuwa ni kuhani. Lakini je! mlitambua? Mungu asingemruhusu nabii huyo kujichanganyisha na madhehebu yao. Baba yake angalimpeleka kwenye shule yao ya theolojia, kwenye dhehebu *fulani* kuu, amfanye mhudumu mzuri, mwajua, na kumfundisha vilivyo, na kumpa upuuzi chungu nzima asiopaswa kuwa nao. Bali Mungu asingeiruhusu nafsi yake ichafuliwe. Mnaelewa? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Asingemruhusu mtu huyo kujichanganyisha na madhehebu. Hakuwa mfuasi wa lolote la hayo, si madhehebu, la Farisayo, Sadukayo, Herodia, ama chochote kile. Mungu asingeliiruhusu.

176 Yeye alizaliwa kiajabu. Alikuwa ni mtoto wa kipekee. Alikuwa ni nabii. Baba yake alikuwa ni kuhani, bali asingemruhusu kujichanganyisha na wanafiki wao wote, dini za Kifarisayo na kadhalika. Alifanya nini? Alimpeleka huko nyikani na kumfundishia jangwani.

177 Ni mafunzo ya jinsi gani! Amina. Yeye alimfundisha kwa tukio. Hilo ndilo bora kuliko yote, kumjua Mungu. Wakati alipotoka, alijua kile hasa agizo lake lilichokuwa. Mungu alithibitisha agizo hilo.

Alilithibitishia wapi? Mtoni. Sasa, kama unaweza kufanya mbili na mbili. Unaona? Mtoni!

Kasema, "Mimi ni sauti ya mtu aliaye nyikani, 'Itengenezeni njia ya Bwana, yanyosheni mapito Yake.'"

178 Yohana, mtu aliyetumwa kutoka kwa Mungu. Mungu asingemruhusu kujichafua nayo. Yeye alimfundisha nyikani, na Mungu. Alimfundisha sio kwenye shule zao, sio katika theolojia

yao. Kama angalifanya hivyo, yeye angalijawa na upuuzi kama ule mnaotoka nao shuleni leo hii, kila namna ya shule. Sio tu Presbiteri, Baptisti na Methodisti, bali shule za Kipentekoste, ni mbaya vile vile, yoyote ya shule hizo za theolojia, huwatoa huko. Loo!

179 Kuja kwake, Roho alitabiri, kwa Isaya. Kuja kwake, kuja kwa Yohana, kulitabiriwa katika Maandiko. Isaya 40:3 ilisema, "Nitamtuma mjumbe Wangu mbele Zangu, kuitengeneza njia," ama, hiyo ilikuwa ni Malaki 3. Ilisema . . . Malaki 3, ilisema, "Yeye angemtuma mjumbe Wake mbele Zake." Nabii, yule nabii wa mwisho, alinena habari zake. Jambo la mwisho lililonena habari zake. Kumbukeni, Kitabu cha mwisho cha Agano la Kale kilisema ya kwamba Eliya angekuja kwa wana wa Israeli kabla ya kuonekana kwa Masihi.

180 Mko tayari? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Kitabu cha mwisho katika Biblia, Ufunuo, kinatuonyesha ya kwamba kutakuwako na kurudi kwake katika siku ya mwisho, kwa kanisa la Kimataifa, ishara. Jinsi wanavyolikosa! Yeye ametabiriwa kuja tena, kabla tu ya kule Kuja kukuu kwa Bwana mara ya pili. Katika Mal- . . . Katika Malaki mlango wa 4, katika Ufunuo pia, mlango wa 3, inatwambia ya kwamba yeye atakuwa hapa katika siku za mwisho. Yeye yule, atakayesimama katika pengo kwa ajili ya watu, akiwa na kundi dogo ambalo Mungu atampa, yeye atakuja katika siku za mwisho. Mungu alisema hivyo. Yeye atakuwa ni ishara kwa taifa hili la Kimataifa, ya kwamba wakati wake umekwisha.

181 Na, kumbukeni, wakati atakapojitokeza jukwaani, wakati umekaribia. Na tuombe Mungu amtume. Wakati umekaribia.

182 Mara huduma Yake ilipomalizika, Masihi alijitokeza. Mara mtu huyu mkuu atakapojitokeza katika siku za mwisho, atakapoimaliza huduma yake, Masihi atajionyesha Mwenyewe. Itakuwa hivyo. Wakati umekaribia, kwa hiyo ni afadhali tuombe. Afadhali muanze kuomba.

183 Ishara yake iliyotolewa na Mungu kwa ajili ya kizazi hiki itathibitisha ninii, kile alicho. Kila mtu atajua jambo hilo. Mungu atalithibitisha. Yeye ataonyesha ishara na maajabu kuliko yaliyopata kufanywa duniani, kwake. Simaanishi kutikisika, kutetemeka, na kunena kwa lugha. Yeye atatetewa na Neno la Mungu, kama mtu huyu alivyotetewa. Kwa nini? Alitabiriwa atakuja, katika Malaki 4 na Ufunuo 3, kwa hiyo atakuja. Hakuna kitu kitakachomzuia; yuaja. Amina. Atakuwa hapa. Amina. Hebu watu wainamishe uso wao leo hii na waanze kumlilia Mungu, muone kitakachotukia. Mtamwona akijitokeza katika uweza. Naam, bwana.

184 Kulingana na Maandiko, ishara yake ya Ujumbe itakuwa ni "kuigeuza." Ninii yake itakuwa nini . . . Tutamfahamu kuwa ni nani? Tutajuaje ya kwamba huyo ndiye wa kweli?

185 Mnajua, Israeli waliuliza hilo wakati mmoja, katika Kumbukumbu la Torati, mlango wa 20…kifungu cha 20, ninaamini ndicho. Alisema, "Tutajuaje kwamba huyu atakuwa ndiye wa kweli?"

Tunajuaje? Mungu anatwambia tutamjua. Atafanya nini? "Atakuwa akiigeuza mioyo ya watoto iurudie Ujumbe asilia wa kipentekoste hapo mwanzo." Loo, jamani!

186 Ishara iliyopuuzwa, ile ishara halisi, nao wanaikosa. Wanaikosa daima.

187 Rudini kwenye Kanisa la kweli, Ujumbe wa kweli! Yeye atasimama peke yake dhidi ya madhehebu, jasiri na asiyeogopa, akiwa na BWANA ASEMA HIVI. Hatapatana na dhehebu lolote. Hatakuwa na uhusiano wowote na lolote; hatawabembeleza kwa chochote. Atakuwa moja kwa moja kwenye Neno, BWANA ASEMA HIVI. Mungu ataithibitisha huduma yake kwa ishara na maajabu, ufunuo mkuu wa Neno, na kulileta kwa watu. Ni siku ya jinsi gani inayokaribia! Kama vile…Atasimama kama vile Petro na Yohana walivyofanya, baada ya, kwenye Siku ya Pentekoste.

Baada ya Pentekoste, ambapo walikuwa wamejazwa na Roho Mtakatifu, wakabatizwa kule, walisimama katika ile mahakama ya Wazee. Walisimama pale kwa ujasiri wote mtu ungaliweza kusimama nao. Wakati, wao walisema, "Tunawakataza kufundisha katika Jina la Yesu Kristo, tena."

188 Akasema, "Ni haki kwetu kuwasikiliza ninyi, ama Mungu? Jiamulieni wenyewe, wasio na elimu, wasio na maarifa." Amina. Walikuwa ni manabii. Walikuwa ni manabii waliotiwa mafuta na Mungu. Walikuwa ni ishara za Roho Mtakatifu. Walikuwa ni manabii. Walijua.

189 Walikuwa tu kama Yohana. Walishakuwa huko kwenye Pentekoste nao walikuwa wamepata kitu fulani.

Hawakuwa kama wengi wa wahubiri wetu leo hii, wa namna yao, wenye kujigamba juu ya dhehebu kubwa tulilo nalo, ni wangapi tulio nao katika makundi yetu makuu. "Tunasimama kama dhehebu kubwa. Tunafanya kazi kuu ya umishenari." Loo, rehema. "Loo, tuna umati mkubwa kuliko hao wengine wote." Ni kitu gani? Ni mvuto wa kisiasa. Ninawatakeni msikilize kwa makini, dakika mbili ama tatu zifuatazo. Mvuto wa kisiasa.

190 Hakika nimesema jambo fulani, dakika chache zilizopita, mnajua kile ninachozungumzia. [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ishara ambayo imetabiriwa. Niliachana nayo, nikaiweka pajani mwenu. Mnaona? Vema, sio ninyi tu hapa, bali kwa wale watakaosikia. Liko pajani mwenu. Fanyeni nayo lolote mtakalo. Ombeni, na mumwangalie Mungu akijitokeza jukwaani. Mwangalieni akilitimiza Neno Lake. Yeye anangojea.

191 Wakati mabomu ya atomiki, nao watu wametishika. Nao Pentagon, hawajui la kufanya. Na ishara za kisiri angani, za visahani virukavyo, na kila kitu ambacho Mungu alitabiri. Wakati wa yule Eliya umewadia, (yeye yuko mahali fulani), akijitokeza jukwaani.

192 Acheni watu, hebu kundi hilo dogo, maskini hao masalio ambao Mungu atampa, hebu maskini hao masalio waanze kumwita Mungu, mwone litakalotukia. Kutakuwako na shindano la kitaifa la kuamua. Kutakuwako na uweza ambao hawajawahi kuuona hapo awali. Shida yake ni kwamba, wakati huu, watakuwa wamechelewa sana. Milango itafungwa. Kwa hiyo, kumbukeni, tuko katika wakati wa mwisho. Ombeni.

193 Angalieni siku hizi tunachokiita huduma. Tuna kitu gani? Sasa, katika kufunga, ninataka kusema jambo hili. Tuna kitu gani? Hatuna kitu. Baadhi ya viongozi wetu walio wakuu sana, wainjilisti wetu walio wakuu sana; mmoja wa wainjilisti wetu aliye mkuu alisema, "Kama ninaweza kupata asilimia kumi ya waongofu wangu wameshikilia, mwaka mmoja, nitashukuru sana." Wakati, hata si mbali sana huko nyuma ambako Finney, alikuwa na asilimia tisini na saba wao.

Paulo alikuwa na mia moja, pamoja na mamia, mamia kuongeza mamia. Mmoja aliokolewa, na, yeye alijazwa sana, ndugu, alienda na kumwambia mtu mwingine; yeye akamwambia mtu mwingine; naye akamwambia mtu mwingine; ikaendelea ikafikia mamilioni. Kwa nini? Walikuwa na kitu. Walikuwa kwenye Neno.

194 Leo hii, tunawazia tu juu ya umati mkubwa. Ni kitu gani? Ni shirika la kisiasa. Kama tukija, mwinjilisti mkuu ajapo jijini, ni kitu gani kinachokuja kwanza? Kundi la watu, kama Wamethodisti wote, Wabaptisti, Wapresbiteri, wote hao. Wanafanya ratiba ya kwamba, hao, "Yeye anaweza tu kuhubiri *hili*, wala hawezi kuhubiri *hilo*. Wala hawezi kuhubiri *hili*, bali anaweza kuhubiri *lile*." Mna kitu gani?

195 Nao wanapanda pale juu, wanawake. Ninazungumza juu ya Wapentekoste. Wanawake wanaingia mle, huko madhabahuni, wanaendelea kusihi.

196 Daima nimepinga wito wa madhabahuni. Afadhali niliseme. Siiamini. Hakuna kitu kama hicho katika Biblia. Mtu yeyote anawezaje kuja 'sipoitwa na Mungu? Usingeweza kumzuia. Haikubidi kuita chochote. Mungu amemwita. Wito wa madhabahuni ni wazo la Kimethodisti. Hiyo ni kweli. Miito ya madhabuhuni, wao wanawashika, wanasema, "Yohana, unajua, mama yako alikufa muda mrefu uliopita."

197 "Loo-loo-loo, naam, ndugu, loo-loo!" Huo si wongofu.

198 Hapa, siku chache zilizopita usiku, tulikuwa na maonyesho huko Louisville, ya mwanamke aliyeletwa kwenye jeneza, akawekwa kwenye jukwaa la kijeshi. "Mamia ya watu," kasema,

"kimbieni madhabahuni." Injili si tishio. Si kuonea huruma. Ni kuongoka kwa imani.

199 Iangalieni mikutano hii, hawa wainjilisti mashuhuri, na hata katika huduma yangu nyenyekevu, bila ya kujiondoa mwenyewe. Wakati mwingine hujisikia kama kuona aibu, nikitoka nje. Hiyo ni kweli. Tunapaswa kufanya nini? Kusimama na kufanya wito wa madhabahuni na kuwashawishi. Wasichana wadogo wanakuja pale, na wote wakitafuna chingamu, wakisema, "Mnaona? Mnaona? Ninaenda. A-ha." Wanawake hawa wanakuja pale, wakiwa na nywele zilizokatwa na nyuso zilizopakwa rangi, Wapentekoste, nao wanaingia, kisha wanatoka, na kusema walinena kwa lugha. Wala kamwe hawaziachi nywele zao zikue, na wangali wanafanya jambo lile lile walilofanya. Ati mwaniambia huo ni wongofu? Huko ni kumdhihaki Mungu. Biblia ilisema, "Ni dhambi na aibu kwao kuzikata nywele zao." Mwanamke aliyekata nywele zake anawezaje kumhukumu mwanamke aliyejipaka rangi usoni mwake? Afadhali mlisikie. Saa yaja, hata shoka limewekwa kwenye shina la mti. Na kila mti usiozaa mema hukatwa.

200 Kuna shida gani? Ilikuwa kosa. Maana, watu wetu wa kisasa, *wanaojiita* wahubiri huku nje, umati mkubwa na watu wanaojigamba. Madhehebu hayajui zaidi kumhusu Mungu kuliko Mhotentoti anavyojua hekaya za Kimisri, inapofikia. Wanapanda huko juu . . .

201 Vipi kama hao watu kwenye Pentekoste wangalipanda huko juu na kusema, "Sasa, Yesu alituamuru ya kwamba tunapaswa kupanda hapa juu na kukaa mpaka tutakapopokea uweza utokao Juu. Sasa, ndugu zangu, tumekuwa hapa siku tisa, tayari. Hebu na tulipokee, kwa imani. Sasa, tuna Roho Mtakatifu. Tutoke, kwa kuwa tumekuwa hapa. Tumefanya yale Yesu aliyotwambia kufanya"? Kamwe kusingekuwako na tukio lolote.

202 Hebu niwaambieni jambo fulani. Ninajua hili liko kwenye kanda, bali hili hapa linakuja, hata hivyo. Sikilizeni. Nitawaambia jambo fulani. Ni aibu. Watu wakijaribu kuninii . . . Kamwe sijapata kuamini ya kwamba Roho Mtakatifu alikuwa "kutetemeka." Sijapata kuamini ya kwamba Roho Mtakatifu alikuwa "ni ushuhuda wa kunena kwa lugha, au kulia, ama kupiga makelele." Hizo ni hisi za mihemko. Ninaamini Roho Mtakatifu anaweza kufanya hivyo. Bali Roho Mtakatifu ni Mungu anayekaa katika mwili. Ninaamini kundi kubwa la watu wanaodai kuwa na Roho Mtakatifu hawajui jambo moja kumhusu. Unakutana na Mungu. Vipi? Siku ya Pentekoste!

203 Hao wanasema sasa, kama vile Wabaptisti leo hii, Wapresbiteri na Wamethodisti.

Niliuliza, "Je! mnaamini mna ninii . . . "

204 "Loo, naam, tunamkubali, kwa imani." Kwa imani, bure! Huyo siye. Ni mhemko.

205 Unataka kuona jua likitua. Unasimama na kuliangalia jua likitua, nawe ulie, na machozi yatiririke chini. Huyo si Mungu. Huo ni mhemko, kutokana na kitu kilicho ndani yako. Unasikia kwamba mtu fulani ni mgonjwa, ama mtu fulani anakufa, unapiga nduru na kulia. Huyo si Mungu. Huo ni mhemko wa kibinadamu. Jinsi ambavyo Mungu . . .

206 Nimewaona watu kwenye mchezo wa mpira, wakifurahi sana wangeigugumiza midomo yao, chochote kile. Usiniambie.

Tunahitaji uamsho, wokovu. Nao wapentekoste wanakuja huku, wanawachochea watu, na kuwaambia, "Wanaponena kwa lugha, wana Roho Mtakatifu." Na baadhi yao wanaishi kila namna ya maisha, baadaye.

Sikiliza, ndugu. Kwenye Siku ya Pentekoste, haikuwa hivyo. Hawakutegemea lugha wala chochote kile. Walipokuwa pale, wamesimama mahali pamoja, kwa nia moja, Mungu alishuka, kihalisi, miongoni mwao. Waliona, juu ya kila mmoja wao, ndimi za Moto, karibu *hivi*, zikining'inia juu ya kichwa chao. Mungu alikuwa pale. Haikuwa ati, "Mkubali kwa imani, ama mhemko fulani." Walijazwa na Roho Mtakatifu, ndipo wakatoka na wakaanza kunena kwa lugha. Lakini, kwanza, walikutana na Mungu.

Hiyo ndiyo shida ya siku hizi. Watu wanachochewa na kusisimkwa, mhemko, wala si Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu ni Mungu anyekaa katika mwili. Maneno yako ni Maneno Yake. Nawaambia, tunachohitaji leo hii, ni wito.

207 Watu huingia, wanawake namna hiyo, wanaingia, wananena kwa lugha, wanatoka nje. Nawe ukienda mahali pao walipo na makanisa yao . . .

208 Laiti Billy angalikuwa ameketi hapa. Ndiyo kwanza nipate barua kutoka huko chini mahali fulani, hivi majuzi, ambapo mwanamke fulani alisema, "Mimi ni mfuasi wa moja, lililo mashuhuri," dhehebu lililo kubwa kuliko yote ya Kipentekoste, shirika kubwa la utatu. Wao walisema, "Wanawake wetu wote, Ndugu Branham, wote hukata nywele zao. Nilikuwa na nywele ndefu nyeusi." Akasema, "Daima nilizipenda, kwa kuwa niliamini lilikuwa ni la Bwana." Kasema, "Sikuwahi kamwe kujipodoa. Kanisa letu linafundisha ati huo ni mtindo wa kale." Kasema, "Wananiambia, nilipokuwa nimezifingirisha nywele zangu katika fundo, kisogoni, kasema, 'Angalia, una tairi iliyotoka pumzi nyuma yako,' na mambo yote kama hayo. Kasema, 'Umebeba ninii iliyotoka pumzi—tairi isiyo na pumzi nyuma ya kichwa chako.'" Kisha kasema, "Hatimaye, mume wangu akasema, 'Mbona usizikate nywele zako ufanane na hao wengine.'"

Sasa nina barua ninayomtumia.

Yeye alisema, "Je! ni kweli? Nilisikiliza moja ya kanda zako, ya kwamba ubatizo wa Kikristo ni katika Jina la Yesu Kristo." Sasa, mnajua kile atakachopata. Sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Yeye alisema, "Niambie, Ndugu Branham. Nina njaa. Ninataka kujua kile nimefanya."

209 Nitasema, "Aibu kwa huyo mume wako aliyerudi nyuma. Na kundi hilo ovu unaloabudu nalo, toka kati yao." Kweli. Mungu hawezi kubadilika. Mungu anaposema jambo lolote, Yeye analimaanisha. Sijali ni wahubiri wangapi waliorudi nyuma wanaotaka kupatana, kufanya shirika kubwa ama kundi. Tunahitaji waokozi. Wanaume watakaosimama na kuwaacha wake zao wafanye hivyo, nina matumaini madogo sana katika ujuzi wenu wa kuwa Mkristo. Kweli. Tubuni, la sivyo mtaangamia! Jamani, masalaale!

210 Wanaingia namna hiyo, wanajiunga na makanisa, makanisa ya Kipentekoste, wanarudi wala hawabadiliki hata kidogo; wanabaki kitu kile kile, hawasongi hata kidogo. Loo, rehema. Ni kitu gani? Mayezebeli mamboleo. Kuna mwanamke mmoja tu katika Biblia aliyepata kuupaka rangi uso wake, Naye Mungu akamlisha kwa mbwa. Mayezebeli mamboleo wakiwavuruta akina Ahabu wao kwa ukanda wa shingo, maskini mwanamume yeyote dondoadume ambaye atamwacha mkewe afanye hivyo, avae kaptura na kadhalika, na kutoka nje hapa mtaani na nguo ambazo zinaonekana kana kwamba zimembana sana kama mnyama aliyechunwa ngozi namna hiyo. Na kwenda... Sisemi hilo kwa mzaha. Hapa si mahali pa mzaha. Hili ni Neno la Mungu. Ni kweli. Hakika. Anashuka mtaani, akiwa na nguo inayombana sana, ameivaa, hata hawezi kutembea. Halafu, mtu fulani akitoa tamshi juu yake, nawe unataka kumshambulia. Unapaswa kupigwa kofi la taya lako, hiyo ni kweli, kwa kumruhusu afanye hivyo. Inaonyesha maumbile yako yametokana na nini. Hiyo ni kweli kabisa.

211 Tunachohitaji ni Injili. Mungu, inua mtu fulani jukwaani ambaye atarudi moja kwa moja kwenye Neno. Mungu alisema hata si jambo la heshima kwa mwanamke hata kuja kanisani na kuomba akiwa amekata nywele zake. Naye mwanamke anayezikata nywele zake, ni...mwanamume ana haki kamilifu ya kupata talaka kutoka kwake. Yeye ni mwanamke mwenye sifa mbaya. Biblia ilisema hivyo. Yeye hamheshimu mumewe. Huenda asijue hilo. Mwanamke yeyote atakayevaa kaptura ana sifa mbaya. Huenda asijue hilo. Mama, sijaribu kukuudhi. Ninajaribu kukuokoa na ziwa la moto, na kuzimu. Tubuni!

212 "Loo," unasema, "ninaye Roho Mtakatifu." Halafu unafanya hivyo, ukiwa na Mungu aliyefanya maskani ndani yako, Mungu yeye yule aliyesema usifanye hivyo?

213 "Loo," unasema, "nilinena kwa lugha." Nimeona pepo wakinena kwa lugha. Nimeona, huko Afrika, wakinywa

damu kwa fuvu la kichwa cha mwanadamu, na kunena kwa lugha na kumwita ibilisi. Nimekuwa kwenye kambi za wachawi na walozi, ambako walinena kwa lugha na kuzifasiri. Nimeona penseli zimewekwa mezani na kuandika katika lugha zisizojulikana, naye mtu huyo anajitokeza, anazifasiri. Ilikuwa ni kweli. Usiniambie kuhusu lugha. Tunazo nyingi kupita kiasi sasa.

Hata hivyo, ninaamini Mungu ana lugha isiyojulikana. Ninaamini ya kwamba Mungu hunena kwa lugha zisizojulikana, bali usitegemee hilo. Paulo alisema, "Nijaposema kwa lugha ya wanadamu na ya Malaika, na sina Roho Mtakatifu, mimi si kitu hata hivyo. Nijapohamisha milima . . . "

214 Watu wengi wanajaribu kusema, "Loo, *huyu* ni mtu mashuhuri wa Mungu. Unapaswa kuona ile miujiza mikuu." Mbona, pepo huponya . . .

Pepo hutoka wanaenda na kufanya mambo kama hayo. Ninajua wachawi wanaotoka, na mambo kama hayo, amejizungushia leso namna *hiyo*. Wanaweka fedha ndani. Anatoa nywele kutoka nyuma ya kichwa chake, anazilowesha damu na kuzitupa ndani. Nao hao watu ni watu waaminifu, wanaamini. Sio mtu huyo. Ni hao watu wanaoamini ya kwamba wanamkaribia Mungu, kupitia kwa huyo mchawi.

215 Hivi Yesu hakusema, "Wengi watakuja Kwangu siku hiyo, na kusema, 'Nimekuwa na miamsho mikuu ya uponyaji'"? Hiyo siyo ishara. Ni ishara ya kwamba tumefika mwisho. Hivi Yesu hakusema, katika Mathayo mlango wa 24, karibu na kifungu cha 24, pia, 24:24? Naye akasema, "Manabii wa uongo watainuka katika siku za mwisho na kuonyesha ishara kuu hata ingewapoteza walio Wateule kama yamkini." Bali Wateule wanasimama kwenye Neno. Wanajua kwamba ishara ya kweli ni nini.

216 Mtu anawezaje, ambaye anafanya mambo haya, ambaye anaikana Imani ya Mungu, kusema ya kwamba yeye ni nabii aliyetoka kwa Bwana? Mtu anawezaje kamwe?

Huenda akawa ni nabii, kama wale waliokuwa huko chini katika wakati wa Ahabu na Yehoshafati, wakati Mikaya aliposimama. Bali walikuwa na mmoja huko chini aliyelitetea Neno, Eliya. Neno la Bwana liliandikwa, ya kwamba Ahabu angeufikia mwisho wake, nalo ono la Eliya liliambatana na jambo hilo.

217 Na mtu yeyote, mtu yeyote anayejiita wa kiroho ama nabii, hukubali kwamba kila Neno la *Hili* ni kweli. Anawezaje kuwa ni wa utatu? Anawezaje kubatiza katika jina la "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu," na kusema ya kwamba ametiwa mafuta na Roho? Anawezaje kuwafundisha watu kosa hilo, na angali awe ametiwa mafuta na Roho? Haiwezekani kutendeka. Ni jambo lisilowezekana.

218 Ninatambua ya kwamba hilo halipendwi na watu. Bali hatutaki kupendwa na watu. Unataka kuwa mwaminifu.

Sasa, Yezebeli na akina Ahabu. Naam, bwana.

219 Kwa nini, ni kwa nini wanafanya jambo hilo? Ni kwa nini hao wanawake wanafanya, wanakata nywele zao, na kujipodoa, na kutoka nje na kuvaa kaptura wakati wanaume wakipitia pale, na mambo kama hayo, waume wao wanafanya hilo? Ni kwa kuwa hawana nabii wa kweli mimbarani mwao, kuwaambia Ukweli. Wao huwaambia, "Vema, hilo si tofauti. Hilo ni sawa. Haiwabidi kutii *hilo*." Ninyi!

220 Ni Neno la Bwana. Biblia ilisema, "Mwanamke yeyote atakayevaa vazi limpasalo mwanamume ni chukizo mbele za Mungu." Mungu habadiliki. Anawezaje kubadilika na awe ni Mungu? Yeye hana kikomo.

221 Wanahitaji nabii wa kweli anayewaambia ya kwamba hiyo ni ishara ya mwisho. Biblia ilisema wangefanya hivyo. Isaya, mlango wa 5, ilisema wanawake wangefanya hivyo katika siku za mwisho. Kweli kabisa. Kwa hiyo, hao hapo.

222 Lakini wanasema wana nabii mimbarani, anayeliogopa Neno la Mungu. Sio . . . Yeye analiogopa kusanyiko.

Na tumwombe Mungu atutumie Nuru hiyo ya vuli, hizo Nuru za jioni, atutumie zile alizoahidi kututumia, kwa Kanisa lililoteuliwa, ambalo litawaambia lililo Kweli, litakalosimama kwenye Neno la Mungu. Awaache Mayezebeli na Maahabu, ndipo watawatenganisha. Hiyo ni kweli kabisa.

223 Kumbukeni wakati wanawake watakapoanza kutenda namna hiyo. Sasa rejeeni nyuma kidogo tu, wakati walipoanza kukata nywele zao na kutenda namna hiyo. Wakati wanawake watakapoanza kutenda jinsi hiyo, ni kwenye wakati huo na msimu huo ambapo Eliya katika siku za mwisho anapaswa kujitokeza jukwaani akiwa na ishara ya wakati wa mwisho, akiwa na ishara ya wakati wa mwisho kama ilivyokuwa katika siku za Lutu. Mnaona? Ishara ya wakati wa mwisho; wakati wanawake watakapoanza kutenda namna hiyo. Wanatenda hivyo sasa. Ni kwenye wakati huo ambapo Elisha atajitokeza jukwaani, akitafuta-tafuta na kuita, akikemea na kurarua, kweli, akiwa na ishara ya Mungu nyuma yake, akiendelea. Yeye hataliita kundi kubwa sasa. Biblia ilisema, "Msiogope, enyi kundi dogo, Baba yenu ameona vema kuwapa Ufalme." Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli kabisa.

224 Hana budi kukataliwa na wote ila lile kundi dogo, kwa kuwa Yeye ni kama Eliya akiwa na mia saba wake, na Yohana akiwa na kundi lake dogo. Naam.

225 Mnaona mahali ambapo tumesimama leo hii? Hatuna budi kurudi kwenye Pentekoste asilia. Hatuna budi kurudi

kwenye mambo ya Mungu. Hatuna budi kurudi. Ndugu, dada, msidanganyike katika ujuzi wenu. Tuna—tunaingojea ile saa.

226 Msichukue tu, "Ni—ninatumaini ndivyo. Ninaamini, kwa imani ninalikubali." Usifanye hivyo. Wewe kutana na Mungu, uso kwa uso, nawe ujazwe na Roho, ndipo uone litakalotukia. Na iwapo roho hiyo iliyo ndani yako ni kinyume na Neno hili, basi achana na hiyo roho. Nenda ukampate . . . Mwombe Mungu akupe Roho, basi.

227 Wakati Roho hii itakapoinuka katika siku za mwisho, itakuwa ni onyo dhidi yao, hao walio wa uongo. Mnaona? Kwa sababu, Yohana alisema, "Msiwazie kusema nafsini mwetu ya kwamba sisi, ya kwamba ninyi 'mnaye Ibrahimu baba yetu.'" Tuna ninii . . . Sisi ni . . .

"Sisi, baba zetu walikuwa ni Wamethodisti, Wabaptisti, Presbiteri, ama Pentekoste." Msiwazie kusema, ninyi, "Mungu," nanyi ni watoto wa Ibrahimu, kwa kuwa Mungu anaweza kutoka kwa mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto. Usiwazie kwa kuwa wewe ni Mpentekoste, ya kwamba utaachiliwa. Si hata kidogo. Mungu anaweza kutoka kwa mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto. Hiyo ni kweli kabisa. Naam, bwana.

228 Nena tu Neno la Mungu, katika ukweli wa siku ya mwisho, ndivyo unabii wake ulivyo.

229 Mkiniruhusu nirejee tu hapa nyuma kwa dakika moja, hebu niwaonyeshe jinsi tunavyoweza kutafuta kujua. Nina Maandiko mengi yaliyoandikwa hapa. Nimekuwa tu nikiyarejea. Ninataka kuwasomea moja. Kutoka, hebu, kwanza, hebu tuchukue . . . Hebu tuchukue Kumbukumbu la Torati, mlango wa 18, nasi tutaona, kwa dakika moja tu. Ili kwamba, kabla hatujafunga hapa, ili kwamba niweze kuwasomea Andiko hili. Katika Kumbukumbu la Torati, mlango wa 18, vema, na hebu tuone sasa. Kifungu cha 20 cha mlango wa 18, Kumbukumbu la Torati, 20.

> *Lakini nabii atakayenena Neno kwa kujikinai kwa jina langu, ambalo sikumwagiza kulinena, au atakayenena katika jina la miungu mingine* (wingi), *nabii yule atakufa.*

Hiyo ni kweli. Amekwisha kiroho. Vema. "Nafsi itendayo dhambi, itakufa." Tuna Mungu mmoja, sio "Miungu."

> *Nawe* ukisema *moyoni* mwako, *Tutajuaje neno* alilo . . . *asilonena Bwana?*

"Tutajuaje? Kutakuwako na wengi sana wa hao, tutajuaje? Huyu anasema *lile*, mwingine anasema *hili*; kama mmoja anasema *hili*, na huyo mwingine alisema *lile,* na kadhalika." Sasa angalia. Tunajua.

*Atakaponena nabii kwa jina la* Bwana*, lisifuate jambo lile wala kutimia, hilo ndilo neno asilolinena* Bwana*, kwa kujikinai amelinena huyo nabii, usimwogope.*

230 Ikiwa Mungu hajalisema, basi usiliogope. Hilo, hilo ni sawa, endelea tu na ulisahau. Unaona?

231 Sasa angalieni yale tunayosikia siku hizi. Kanuni ya Imani ya Mitume, kanuni ya imani ya Methodisti, kanuni ya imani ya Baptisti, kanuni ya imani ya Wapentekoste, kanuni ya imani, kanuni ya imani, kanuni ya imani. Kanuni ya imani ni nini? Unazipata wapi? Ninampa changamoto mtu yeyote anionyeshe Kanuni ya Imani ya Mitume katika Biblia. Ninaamini hakuna kitu kama hicho.

Kama mitume walikuwa na kanuni yoyote waliyopata kushikilia, hii hapa: "Tubuni kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa maana ahadi hii ni kwa ajili yenu."

Hivi hamwoni mahali tulipo, enyi marafiki? Tuko katika hali mbaya sana. Ni kitu gani? Ishara ya kweli iliyopuuzwa.

232 Sasa, ninyi ni wanaume na wanawake, wengi wenu, nanyi ni watoto wa Mungu. Msilipuuze. Kumbukeni ya kwamba tunapaswa kuwa na mambo haya. Yanapaswa kutukia katika siku hii, katika saa hii tunayoishi sasa. Hii ndiyo ile saa, kabla tu ya kule Kuja kwa Masihi, kunapaswa kuwe na tangazo litakalotoka kwa Mungu.

Hebu niwasomee hilo. Hebu turudi kwenye Malaki. Ndicho cha mwisho cha Agano la Kale, na msikilize yale anayosema hapa katika Malaki. Ndipo tunaninii . . . Sikilizeni hili kwa muda mfupi.

Sasa, kama mkiangalia, Malaki 3, ikisema ya kwamba Yesu alinena kuhusu kuja kwa Yohana.

*Angalieni, namtuma mjumbe wangu, naye ataitengeneza njia mbele yangu; naye Bwana mnayemtafuta atalijilia hekalu lake ghafula; naam, yule mjumbe wa agano mnayemfurahia, angalieni, anakuja, asema* Bwana *wa majeshi.*

233 Huyo alikuwa ni Yohana, akikutangaza kuja kwa Yesu. Naye alikuja hekaluni, alivyosema hasa, Mjumbe wa agano, Malaika aliyekuwa pamoja na . . . nyikani pamoja na—pamoja na wale wanafunzi, ama pamoja na Israeli. Je! mnaamini ya kwamba Yeye alikuwa ndiye yule Mjumbe? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] "Vema," Yeye akasema, "Natoka kwa Mungu, Nami ninaenda kwa Mungu."

234 Sasa, ni kwa nini Paulo alipewa ugonjwa? Kumfinyilia chini.

Baada ya Yesu kufa, na kuzikwa, na kufufuka tena; baada ya kitambo kirefu, Paulo alikutana Naye, uso kwa uso, njiani

akienda zake Dameski. (Akasema, “Nimetoka kwa Mungu, na nikaenda kwa Mungu.”) Paulo akaangalia juu. Kulikuwako na Nuru kubwa pale, Nguzo ile ile ya Moto. Mnajua yale ninayonena habari zake? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Nguzo ile ile ya Moto. Naye Paulo akazungumza Naye, Naye akamzungumzia Paulo. Hao watu hawakumsikia. Hawakumsikia. Bali Paulo alimsikia. Akasema, “Sauli, Sauli, mbona wanitesa?”

Akasema, “U nani Wewe, Bwana?”

235 Akasema, “Mimi ni Yesu. Sasa amka uende kwenye barabara inayoitwa Nyofu. Utaambiwa tangu hapo na kuendelea. Ninaye nabii anayepanda kuja huko kukwambia utakalofanya, unaona. Na jinsi ya kuninii . . . ”

236 Paulo akashuka, akabatizwa, na kumwitia Bwana, akampokea Roho Mtakatifu.

Ndipo Paulo akasema, “Nilikuwa na udhaifu mwilini mwangu, niliopewa, ibilisi, mjumbe wa ibilisi, *kunipinga*,” hiyo ni kama, “pigo baada ya pigo.” Angepata nafuu zaidi, kisha anaupata, unamshambulia tena. Kasema, “Nilimtaka Bwana shauri mara tatu, aniondolee, bali Bwana akasema, ‘Paulo, neema Yangu imetosha.’” Kisha kasema, “Nisije nikajivuna kwa wingi wa ufunuo.”

Alikuwa na mengi zaidi, kwa ufunuo, kuliko Petro, Yakobo, Yohana, ama yeyote wao. Yeye alimwona baada ya Yeye kuondoka kwa labda miaka miwili, ama zaidi, amesimama katika Nguzo ya Moto, akizungumza naye. Ni zaidi sana vipi leo hii, miaka elfu mbili, Naye angali hai! Amina.

237 Kasema, “Nilipewa, nisije nikajivuna zaidi, nikisema, ‘Sasa, ndugu, mimi niko juu yenu nyote. Mnaona? Ni—nilimwona baada ya Yeye kufufuka katika wafu, nami nikazungumza Naye. Mimi . . .’ Nisije nikajivuna zaidi ya hapo, nilipewa kitu fulani, kunidumisha mnyenyekevu.” Naam.

238 Yeye ndiye aliyewaambia wabatizwe tena, mara nyingine, katika Jina la Yesu. Kasema, “Kama Malaika kutoka Mbinguni . . . ”

239 Yeye alisema, “Mimi sikwenda kwenye shule zao, popote walipokuwa.” Kasema, “Sikwenda Yerusalemu mara moja, wala sikwenda kwa muda wa miaka kumi na minne.” Kasema, “Nilishuka kwenda Misri, nikashuka katika Asia huko chini.” Naye akamsihi Bwana, alikuwa huko chini kwa muda wa kama miaka mitatu, akilisoma Agano la Kale, akiliona lote likilinganika. Wakati aliporudi, katika muda wa miaka kumi na minne baadaye, akakutana na Petro na hao wengine, naye alikuwa na Injili ile ile, alibatiza vile vile, na kufanya jambo lile lile. Amina. Alijua ilikuwa ni kweli. Naam, bwana.

240 Sikilizeni Malaki sasa, hapa, Malaki 3. Sasa, kama mngeweza, hebu niwaelezee hili waziwazi, ninaamini. Hebu

na tufungue kwa urahisi sasa kwenye Mathayo mlango wa 11. Na tuone kama mimi...Huenda nimelipata hili vibaya. Nafikiri nimelipata. Huenda ikanibidi kuangalia kwanza nilione. Mathayo 11. Hebu tuone. Tuanzie kwenye:

> *Ikawa Yesu* alipokwisha *kuwaagiza wanafunzi wake kumi na wawili, alitoka huko kwenda kufundisha na kuhubiri katika miji yao.*
>
> Na...*Naye Yohana...aliposikia* ya kwamba alikuwa...huko *gerezani matendo yake Kristo,* yalikuwa...*gerezani matendo yake Kristo, alituma wanafunzi wake wawili,*
>
> *Wakamwuliza, Wewe ndiwe yule ajaye, au tumtazamie mwingine?*

Jicho la Yohana la tai liliingia utando, huko chini gerezani. Mnaona?

> *Yesu akajibu akamwambia,* Nendeni...*mkamweleze Yohana tena mambo* haya *ambayo* wewe ninyi... *mnayasikia na kuyaona;*

"Yohana ni nabii. Na ikiwa ata—atasikia hili, yale yanayoendelea, yeye atajua kwamba Mimi ni Nani." Mnaona? Akasema:

> *Vipofu wanapata kuona,...viwete wanakwenda, wenye ukoma wanatakaswa,...viziwi wanasikia,* na *wafu wanafufuliwa,...*

"Na madhehebu yote yako pamoja"? Halisemi hivyo, sivyo? [Kusanyiko linasema, "La."—Mh.] La. Halisemi. Lilisema:

> *...viwete wanakwenda, wenye ukoma wanatakaswa,...viziwi wanasikia,* na *wafu wanafufuliwa, na maskini wanahubiriwa habari njema.*

Hiyo hapo ishara. Angalieni. "Nao walipokwenda..."

> *Naye heri awaye yote* ambaye...*asiyechukizwa nami.*

Sasa angalieni. "Heri awaye yote *asiyechukizwa* Nami," kwa maneno mengine, ama, "'kunionea haya.' Heri yeye ambaye hatanionea haya." Mnaona?

> *...hao walipokwenda zao, Yesu alianza kuwaambia* makutano *habari za Yohana, Mlitoka kwenda nyikani kutazama nini?*

Mwangalieni nabii huyu sasa.

> *...Mlitoka kwenda nyikani kutazama nini? Unyasi ukitikiswa na upepo?*

Sio Yohana. Loo, la. "Enyi uzao wa nyoka nyasini," akayaambia madhehebu hayo, "ni nani aliyewaonya ninyi kuikimbia ghadhabu itakayokuja? Msianze kusema, 'Sisi ni wa *hili* na *lile*, maana Mungu anaweza kwa mawe haya kuwainua

watoto.'" Loo, ndugu, haukuwa ni unyasi ukitikiswa na upepo, kwake yeye.

> . . . *Unyasi ukitikiswa na upepo?*

> Ama *kweli mlitoka kwenda kuona nini? Mtu aliyevikwa mavazi mororo*? (Inambidi kubadilisha nguo zake mara mbili ama tatu wakati akihubiri?) *tazama, watu wavaao* mavazi *mororo, wamo katika nyumba za wafalme.*

Hao ndio wahudumu wanaotoka wanaenda na kuwabusu watoto wachanga, mwajua, na—na kuwaoza vijana, na—na wanaenda shuleni na kutoa hotuba za kiakili, na, mwajua, mambo hayo madogo yote ya kidondoadume. Mnaona? Mnaona? Yeye hautumii upanga wenye mikono miwili hapa nje kwenye mstari wa mbele. "Mlitoka kwenda kuona nini, jamaa fulani kama huyo?" Vema, Yeye anawauliza.

> *Lakini* ninyi *mlitoka kwenda* . . . *kuona nini? Ni kuona nabii?* (Sikilizeni.) *naam,* nami *nawaambia, na aliye mkuu zaidi ya nabii.*

Naam, bwana. Yeye alikuwa ni nini? "Ati yeye ni 'zaidi ya nabii'?" Yeye alikuwa ni nabii, na zaidi. Alikuwa ni mjumbe wa wakati huo.

> . . . *mlienda* huko *kuona nini? Ni kuona nabii? Naam, nawaambia, na aliye mkuu zaidi ya nabii.*

> *Huyo ndiye* . . . *aliyeandikiwa haya, Tazama, mimi namtuma mjumbe wangu mbele ya uso* wangu, . . . *kuitengeneza njia mbele* yangu.

Angalieni hapa katika Malaki 3. "Tazama, ninamtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu."

241 Angalieni. Sasa, Malaki 4, hebu nisome hili. Yeye atakuja tena.

> . . . *angalieni, siku ile inakuja, inawaka kama tanuru; na watu wote wenye kiburi, naam,* . . .

242 Hiyo ni leo hii. Ninatembea barabarani na kuwaona watu hawa. Unaweza kuzungumza nao, nao wanakucheka, wanakudhihaki. Nawazia, ni kitu gani? Hivi majuzi, nilikuwa nikitembea, nikishuka, karibu na majengo hapa chini. Nilikuwa nikizungumza na watu fulani, nao wakasema tu "loo," wakaenda zao.

Kitu fulani kikaniambia tu, "Hao ni chakula cha atomiki, hivi karibuni watakuwa ni majivu yaliyotawanyika ardhini. Achana nao. Umenena amani yako. Jiandae na uondoke hapa." Haleluya! Sikupaswa kusema hilo, nadhani. "Jiandae. Jifunge viuno vyako. Ninakuita." Hiyo ndiyo sababu ninangojea.

*Kwa maana angalieni, siku ile inakuja, inawaka kama tanuru;* naam*, na watu wote wenye kiburi,. . .nao wote watendao uovu, watakuwa* kama makapi*;. . .*

Hilo ndilo litakalotukia hasa. Ni kitu gani kinachotendeka wakati ninii kuu. . .baadhi yenu wakulima; wakati moto mkali unapolivamia shamba la ngano, wakati ni makapi tu? Unayateketeza kabisa, majivu yakiachwa nyuma. Hivyo ndivyo utakavyofanya, wakati ule, wakati utakapoipiga.

*. . .siku ile* inakuja ambayo *itawateketeza, asema* B*WANA wa majeshi; hata haitawaacha shina wala tawi.*

Hawatabaki kitu.

*Lakini kwenu ninyi mnaolicha jina langu, Jua la haki* litawazukia*, lenye kuponya katika mbawa zake;. . .* ninyi *mtatoka nje, na kucheza-cheza kama ndama wa mazizini.* (Huo ni ule Utawala wa Miaka Elfu.)

*Nanyi mtawakanyaga waovu; maana watakuwa majivu chini ya nyayo za miguu yenu; katika siku ile niifanyayo, asema* B*WANA wa majeshi.*

Itatukia, kwenye ule Utawala wa Miaka Elfu. "Majivu ya watendao maovu."

*Ikumbukeni. . .torati ya Musa, mtumishi wangu, niliyomwamuru. . .huko Horebu kwa ajili ya Israeli wote, naam,* amri *na* hukumu.

Sasa, sikilizeni kwa makini sasa.

*Angalieni, nitawapelekea Eliya nabii, kabla haijaja siku* ile *ya* B*WANA, iliyo kuu na kuogofya.*

243 Sasa, hiyo isingewezekana kuwa ni Yohana. Isingewezekana, kwa sababu ulimwengu ungaliangamizwa wakati huo. Lakini hapa Yeye alisema, katika Mathayo 3, Yeye anamtuma mjumbe mbele Zake. Naye Yesu alisema, "Huyo ndiye Eliya aliyekuwa aje, kuitengeneza njia mbele Zangu."

"Lakini kabla bomu hili kuu la atomiki halijapiga, nitawapelekea Eliya nabii."

*Naye ataigeuza* mioyo *ya baba iwaelekee watoto wao, na* mioyo *ya watoto iwaelekee baba zao, ili nisije nikaipiga dunia kwa laana.*

244 Kutabiri, katika siku hii.

Lakini sasa mnasema, "Loo, Eliya huyo, huyo alipaswa kuwa ni Yohana." Mjumbe wa agano alikuwa ni Yohana, kweli. Hiyo ni kweli kabisa. Yesu alisema hivyo, na akalithibitisha papa hapa, "Huyo ndiye niliyenena habari zake." Lakini, mnaona, isingekuwa ni yule Eliya ajaye. Mnaona? Isingewezekana. Kwa kuwa, mnaona, kama angalikuwa ni yeye, basi huo unabii ulikosea; dunia haikuangamizwa huko nyuma. Mnaona? "Lakini kabla haijaja siku ile ya Bwana iliyo kuu na kuogofya,

nitawapelekea Eliya. Naye atarudisha," angalieni kule kuja Kwake mara ya kwanza, "mioyo ya baba iwaelekee watoto wao." Hivyo ndivyo Yeye alivyofanya, kwanza, akauleta ujumbe wa kile kipindi kipya cha wakati, kule kuja kwa Kristo sasa, akiwavuta wale baba wa kiothordoksi kutoka kwenye imani hiyo ya kiothordoksi, na kuwaingiza kwenye imani mpya ambayo ilikuwa ndiyo kwanza izaliwe.

Ndipo wakati atakapokuja mara ya pili, "Na mioyo ya watoto iwaelekee wale baba wa kipentekoste, ule Ujumbe wa asili."

245 Sasa fungueni hapa kwenye Ufunuo 3, nanyi mtaliona pale pale tena. Kwa hiyo, imetabiriwa. Tuko kwenye wakati wa mwisho, ndugu yangu. Hiyo ni kweli.

246 Ni kama wale manabii mia nne dhidi ya Mikaya, wao wanasema tunaninii. . .Tuko katika siku hiyo ya mwisho, tunajua. Nabii wa uongo, anaonyesha ishara za uongo, kujiunga na madhehebu. Wao wanasema, "Njoo ukajiunge. Hebu na tujiunge. Wewe njoo ukajiunge na kanisa letu. Leta uanachama wako. Tuko tayari asubuhi ya leo ili uweze kuuhamisha ushirika wako kutoka kwenye kanisa *lile* uulete kwenye *hili*." Loo, upuuzi. Uanachama wako unakufaa nini? Kama huna urithi Mbinguni, sahau hilo. Manabii wa uongo wataonyesha ishara za uongo.

247 Lakini, angalia, manabii wa kweli, watadumu na Neno la Mungu. Ishara za kweli zitazaa Neno la kweli la Mungu kwa Kanisa la kweli, nalo Kanisa la kweli litalipokea Neno na kulifurahia. Wakati lile kundi dogo, litakalototolewa katika siku za mwisho, ambalo litakuwa ni masalio ya Mataifa, yatakayovushwa ng'ambo ya pili.

248 Wakati Yesu alipokuja, hakukuwako—hakukuwako ila na wachache sana kule walioamini. Kundi dogo la Yohana ndilo lililoamini. Yesu aliwachukua tangu hapo na kuendelea, akawafanya hao kuwa wanafunzi na kuendelea. Wakati Eliya. . .

249 Wakati maangamizi yalipotokea, hapo wakati wa Nuhu ulipokuja, yeye alikuwa ni ishara, naye akawaingiza watu kwenye safina. Wakati Eliya alipokuja, aliwaondoa watu kutoka kwenye machafuko waliyokuwa ndani yake. Wakati Yohana alipokuja. . .Manabii wote walikuwa ni ishara, ishara, ishara, ishara.

Naye alituahidi ishara katika siku za mwisho. Katika siku za mwisho kutakuwako na ishara. Ni ishara iliyopuuzwa. Watu hawaioni. Wanairuka tu, na kuiachilia. Ndugu, dada, usijiunge na kanisa. Hebu niseme jambo hili, katika kufunga sasa.

250 Kama umekuwa tu na tukio la mhemko fulani, kuchochewa, usiutegemee huo. Usifanye hivyo, kwa ajili ya watu wako. Wewe ni. . .Ninawazungumzia watu. Niliwasikia wakivifungulia

vinasa sauti kule nyuma, wakati uo huo. Ninalizungumzia Kanisa sasa. Mnaona? Sikilizeni. Msifanye hivyo.

251 Mimi husema mambo hayo mengi wakati mwingine, namna hiyo, kusudi watu walio nje nchini hapa nje, wadumu na Mungu. Iangalieni ishara yenu ya kweli. Mtaiona. Itakuwa kote karibu nanyi, bali mamilioni watatembea papo hapo karibu nayo wasiione.

Wakati Yesu alipokuja, hawakumjua.

Hawakumtambua Eliya. Unajua walichosema wakati Eliya alipopaa juu? Hawakuamini upuuzi huo. Walisema, "Ni upuuzi." Wale watoto pale pale kwenye ule, mji wake mwenyewe ambako aliishi. Aliishi humo, akahubiri humo, akafanya ishara na maajabu mumo humo kwenye nchi hiyo. Wakati kamsa ilipopigwa, "Hatuwezi kumpata Eliya; Bwana alimtwaa juu kwa upepo wa kisulisuli," walilicheka jambo kama hilo.

252 Huyu hapa anakuja Eliya, Elisha, akiwa na ishara zile zile juu yake, mfano wa Kristo na Kanisa Lake. Huyu hapa Eliya anakuja, yeye yule; Elisha, ishara zile zile alizokuwa nazo Eliya, akishuka moja kwa moja, akizifanya hizo. Hata watoto wao wadogo walimfuata, kasema, "Mzee kipara, mbona hukupaa juu kama Eliya?" Mnaona kilichowapata hao watoto wasio na kicho?

Leo hii wanacheka na kufanya mzaha. Usijali, ndugu, hukumu imening'inia angani sasa hivi. Imeandikwa kwenye uso wa kila Mmarekani. Hiyo ni kweli. Hukumu inaning'inia angani, hasira yote ya Mwenyezi Mungu.

253 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] "Wasiowapenda walio wema; wenye mfano wa utauwa, bali wakikana nguvu zake: hao nao mjiepushe nao."

254 Kamwe usichukue msisimko. Usichukue mhemko. Usichukue chochote mpaka utakapokutana na Mungu, uso kwa uso, na umruhusu Roho wa Mungu aingie ndani yako. Ataujaza moyo wako na nafsi yako kwa uweza, na upendo, na kuuwasha moto.

255 Mungu, nisaidie nipapate mahali pangu huko ng'ambo, mahali fulani katika siku chache zijazo, hapo nibaki mpaka nitakapoona mahali hatua yangu ya pili ilipo.

256 Tumengojea muda mrefu. Nimengojea muda mrefu. Ninakumbuka nikikata nyasi kwenye kitalu changu huko nyuma. Nilipoijenga nyumba hii hapa juu, Bwana aliniita. Mke wangu alilia kwa kuwa hakutaka kumwacha mama yake. Kasema, "Labda hatatunzwa."

Nikasema, "Ninaye mama mkongwe, pia."

257 Nilikuwa nimeketi pale chini, siku moja, nikikata nyasi. Nikaketi chini. Kwa udhahiri kabisa, Sauti ilikuja, ikasema, "Jitenge, ndipo nitakubariki."

Nikasema, “Bwana Mungu, nifanye nipate furaha hapa. Unaona yale yanayonikabili.”

258 Mambo hayo yote yamekwisha sasa. Mama Broy yuko Utukufuni; Mama Branham, pia.

“Nielekee wapi, Bwana?”

259 Hukumu itaipiga nchi hii, moja ya siku hizi. Yapo mataifa mengine ambayo hayajaisikia Injili. Kuna mahali kwingi.

260 Lolote ufanyalo, usiyasahau maneno yangu. Usiyasahau. Hebu hili litie nanga. Mungu na achukue kalamu ya chuma na kuliandika moyoni mwako, usije ukalisahau. Usilisahau. BWANA ASEMA HIVI. Mrudieni Mungu, kwa mioyo yenu yote. Rudini. Msitegemee mhemko, mwasho, au chochote kile. Mtafuteni Mungu kwa yote yaliyo ndani yenu, mpaka jambo fulani liwapate, kwamba mnataka kunyosha mambo, mnataka kuwa watauwa, mnamcha Mungu, m—mnataka kuishi maisha mazuri. Fanyeni hivyo. Kamwe msisahau hilo, kwa kuwa tuko katika wakati wa mwisho. Sasa, kumbukeni, tuko katika wakati wa mwisho.

261 Na mkumbuke jambo hili, ninapofunga, kuomba, katika dakika moja. Msisahau. Nisikieni, enyi maskani. Kama kanda hii ingali inaendelea, nisikieni, enyi walimwengu, mahali itakapoenda. Ishara itatokea, ishara ya kweli. Labda imeinuka tayari nayo imepuuzwa, ishara ya kweli ambayo Mungu ameitoa daima, ambayo imepuuzwa.

Na tuombe.

262 Yesu wa Nazareti, kama vile ile Sauti kuu ilivyonena huko ng’ambo siku ile, majuma machache yaliyopita, ikisimama karibu nami, wakati nikilivuka lile gogo, kuuzunguka ule mti, nayo Roho ile iliyoshuka kupitia kwenye vilele hivyo vya miti na kusema, “Yesu wa Agano Jipya ndiye Yehova wa la Kale.” Ee Mungu, kwenye Mwamba huu ninasimama. Sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao. Sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao.

263 Kwa muda wa miaka thelathini, Bwana, nimelia, kupitia kwenye bonde hili hapa. Ujumbe huo, sijasonga hata inchi moja kutoka Kwake, kutoka mahali nilipoanzia, Ujumbe ule ule tu, jambo lile lile; ukiwaita watu warudi, sio kwenye msisimko, bali kwenye tukio la kukutana na Mungu na kuzaliwa kwa Roho Wake. Loo, ni kitu gani kitakachosalia ila hukumu? Hao wanaoukataa Ujumbe huo, Bwana, hakuna kitu kilichosalia.

264 Wewe umelitimiza sana Neno Lako, kuzitangaza ishara za siku ya mwisho, na kulithibitisha pasipo kukosea, kwamba Wewe ni Mungu, na ya kwamba tupo hapa. Hata wakati tunapowasikia wale wainjilisti wakuu nchini leo, wote wakipaza sauti. Na kwenye makao makuu ya taifa letu, na mataifa mengine yakichagua, na—na kushikwa na hofu. Na

tunapowasikia watu hawa mashuhuri, hata kufikia huko Ufaransa, wakitabiri ya kwamba bomu la kwanza litaangushwa Louisville, Kentucky, kwa mamia ya maili itaenea nchini. Ee Mungu, hao walikuwa na nafasi ya kusikia, bali wasingesikia.

265 Magazeti, vitu vya kanisa, televisheni, redio, zimeutangaza. Hakuna udhuru. Halafu, Bwana, Wewe ulisema, "Wote alionipa Baba watakuja, na hakuna mtu anayeweza kuja asipovutwa na Baba kwanza."

266 Sasa, Baba, ninaomba maombi haya kwa ajili yangu mwenyewe. Mimi hapa, nikifikia kuwa mzee sasa, wala sijui ni siku ngapi tulizobakisha, Bwana. Huenda tusiwe na leo tena. Lakini chochote kilichosalia, Bwana, na kile kilichosalia maishani mwangu, Ee Mungu, hivi inawezekana ukichukue na kufanya jambo fulani nacho, kwa ajili ya utukufu Wako?

267 Kwanza ninajiombea mwenyewe, Bwana, ya kwamba Wewe utanipa mapenzi Yako. Mapenzi Yako na yatendeke, Bwana, hata yawe ni nini. Ninataka isemwe kwenye siku ile nitakapokuja kukutana na Wewe, "Ni vema." Kama ni kubwa, ama ni dogo, chochote kilicho katika moyo Wako mkuu kwa ajili ya maisha yangu, Bwana, mimi hapa.

268 Mtume Malaika na kaa la moto akaisafishe midomo yetu na kututakasa, Bwana, kwa ajili ya kitu kikuu cha mwisho ambacho kinakaribia kuipiga dunia. Jalia tuwe sauti iliayo kwenye nyika la dhambi, "Jiweke tayari kukutana na Mungu."

269 Kanisa hili dogo, watu hawa ambao wanakuja, siku baada ya siku, na kuendesha magari mamia ya maili. Ee Mungu wa Ibrahimu, Isaka na Yakobo; wa Milele, mwenye upendo, na asiyesahau hata tendo moja, ambaye alimfufua Yesu katika wafu, na sasa Yeye ameketi kwenye mkono wa kuume wa Ukuu huko Juu; Mungu aliyefanya maskani katika mwili: wabariki watu hawa ninaowabariki katika Jina Lako. Jalia daima wakumbuke na kujua ya kwamba kuna ishara, ishara ya mwisho. Ninaomba ya kwamba utawapa, na kuwafanya washawishi wa wengine: kwenye kazi yao, popote pale walipo, pembeni mwa barabara, vituo vya petroli, ama popote pale walipo, kushuhudia kwenye duka la vyakula, kwa muuza maziwa. Popote pale, Bwana, kama kitu fulani kikiwaonya moyoni mwao, jalia wawe ni shahidi. Jalia waishi maisha ya kitauwa sana na yaliyotakaswa mpaka watakuwa ni nyaraka zilizoandikwa zinazosomwa na watu wote.

270 Mungu, wabariki wanawake wetu. Ee Mungu, ninaomba ya kwamba utawajalia kuosha nyuso zao, wale wasioziosha, waondolee mbali ninii...wajiondolee hivyo vipodozi vya Yezebeli. Jalia wawe na ujasiri wa Wakristo, na Roho wa Mungu juu yao, wa kutosha, kujua ya kwamba hawapaswi kuvaa nguo hizo chafu wanazovaa. Waachilie nywele zao zikue, kama mama wenye heshima. Kwa kuwa imeandikwa katika Biblia, "Lina

thamani machoni pa Bwana lile tawi dogo litakaloepuka upuuzi huu wote unaokuja katika siku ya mwisho. Litakuwa na utukufu machoni pa Mungu," kama vile nabii alitabiri. Mungu, tujalie hilo.

271 Hakuna kitu cha zaidi ninachoweza kufanya. Nimepaza sauti yangu, mwaka baada ya mwaka, Bwana. Na isipokuwa Wewe utende kazi sasa, hakuna jambo ninaloweza kufanya. Ninaomba ya kwamba, ya kwamba utatenda. Nami ninajua Wewe utatenda, kwa kuwa uliahidi hilo katika Neno Lako. Na hapo ndipo ninaposimama. Ninaweza tu kutoa ushuhuda, Bwana. Wala hakuna mtu awezaye kuja usipomvuta Wewe; na wote aliowatoa Baba watakuja. Nina hakikisho hilo, ya kwamba Neno Lako litashughulikiwa. Tubariki, Bwana.

272 Na kama kuna wale hapa ambao wanategemea tu mhemko, labda wamepaza sauti. Labda wana Roho Mtakatifu. Ama, tusingehesabu jambo hilo, Bwana, kwa kuwa tumewaona watu kwenye michezo ya mpira, wakipaza sauti. Tumewaona watu kwenye burudani za kilimwengu, wakipaza sauti. Tumewaona wale walio na furaha sana hata wanalia, huko sakafuni, wakicheza-cheza, na mambo hayo yote. Huyo si Wewe, Mungu.

273 Bali kukutana Nawe na kuzungumza Nawe, Nawe unajibu, hilo ndilo tunalotaka, Bwana. Loo, ninakuomba, Mungu, kwenye dakika ii hii, ya kwamba utamtuma huyo Roho Mtakatifu chumbani, mahali hapa padogo, duni. Hakuna mahali panapomfaa Yeye kuja. Bali naomba, Mungu, ya kwamba, katika njia yako Mwenyewe, ya kwamba Wewe utamtuma sasa hivi chumbani. Akawasadikishe watu.

274 Kama nilivyosema muda mfupi uliopita, Bwana, labda umeliweka jiwe la kujikwaa mbele ya mtu fulani, kuhusu miito hii ya madhabahuni, kuwabembeleza na kuwasihi watu wapande juu. Na tutakaporudi mwaka ujao, tunawakuta ni wana wa kuzimu maradufu kuliko walivyokuwa hapo mwanzo. Wanawezaje kuja usipowaaminisha na kuwasadikisha, Ewe Roho Mtakatifu mkuu?

275 Nami ninakuomba, Bwana Mungu, kama mwenye dhambi huyo mwanamume au mwanamke, mvulana ama msichana, yumo humu jengoni asubuhi ya leo, ya kwamba Roho Mtakatifu atakuja na nguvu kuu sana za kusadikisha hata machozi yatatiririka mashavuni mwao na kumiminika nafsini mwao, Bwana, ili kwamba kutoka kwenye vilindi vya moyo wao watamwamini na kumkubali Kristo. Tujalie, Bwana. Hawatahitaji madhabahu yoyote. Nafsi yao itakuwa ndiyo madhabahu yao. Tujalie, Bwana. Ndipo wanakuja kwa moyo mkunjufu Kwako, na kusema, "Sasa ninataka kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zangu ambazo nimezitubia." Tujalie, Bwana. Wajaze na Roho Mtakatifu.

276 Tupe Wainjilisti ulimwenguni leo hii, sio wale wanaoshawishi na kuvuta, na kuwafanya wana wa kimadhehebu. Mungu, jiinulie watoto. Wafanye watu, Bwana, kuomba. Ninawazia juu ya nyumba ya Kornelio. Halikuwa limetukia kwa Mmataifa hapo kabla, bali walikuwa wakifunga na kuomba. Ndipo wakati mtu huyo wa Mungu, nabii huyo, aliposimama hapo, "Ndipo alipokuwa akisema maneno haya, Roho Mtakatifu aliwashukia hao waliolisikia Neno." Mungu, tujalie mkutano wa namna hiyo. "Petro alipokuwa akisema maneno haya." Ee Mungu, walikuwa tayari. Walikuwa wakifunga. Walikuwa wakingojea. Walikuwa waaminifu. Hawakuwa "wakingojea" tu, walikuwa "wakingojea hata."

277 Hao mitume walingojea hata Mungu akashuka miongoni mwao, nao wangeweza kumwona na kuzungumza Naye. Walitoka wakaenda kwa mioyo iliyouteketeza ulimwengu kabisa. Walikuwa jasiri, nao wakasimama katikati ya mahali ambapo huenda palimaanisha kukatwa vichwa vyao wenyewe. Walisema, "Je! ni haki kwetu kuwasikiliza, ama madhehebu yenu, ama ninyi watu wa kimadhehebu? Ama, tumsikilize Mungu? Jiamulieni ninyi wenyewe." Na moja kwa moja, mara waliporuhusiwa kwenda, walitoka wakaenda moja kwa moja na kulihubiri Jina la Yesu Kristo tena. Ee Mungu, tupe—tupe hao, Bwana.

278 Mwinue huyu unayenena habari zake katika Maandiko, kwa ajili yetu. Mtie mafuta, Bwana. Ninaomba aje. Mtume, Bwana. Ee Mungu, mioyo yetu yenye njaa inalia. Mtume, Bwana, ambaye atawarudisha watu kwenye Imani ya baba zao tena, atakayewaondoa kwenye vibaraka hawa wa kimadhehebu, na kuwaingiza kwenye tukio halisi na Mungu, kama walivyofanya huko Pentekoste, kanisa halisi tena, linalowaka moto, likiwa na Ujumbe ule ule, Imani ile ile, Fundisho lile lile, Biblia ile ile, Mungu yeye yule akiwa na ishara ile ile. Tuinulie nabii, Bwana.

279 Waponye wagonjwa miongoni mwetu leo, Bwana. Wapo wale hapa walio wahitaji. Ninawaombea, Baba. Nimechukua muda mrefu sana, nikikawia asubuhi ya leo, na kuna wale walioketi hapa.

Usiku mmoja, wakati mtume Paulo alipokuwa akihubiri usiku kucha, kijana mwanamume alianguka kutoka humo jengoni, akafa. Aliingia usingizini. Hakutaka kufanya hivyo, bali a—alilala. Naye akaanguka, na uhai wake ulikuwa umeondoka. Ndipo huyo mtume akaomba, nao uhai ukamrudia tena.

280 Ee Bwana Mungu, wapo wengi hapa walioshikwa na maradhi. Na ingawa tumechelewa tukapitisha wakati wa kuliruhusu kanisa kuondoka, wapo wale walio wagonjwa. Ee Mungu, jalia uweza huo, huyo—huyo Roho Mtakatifu ambaye huja binafsi katika Nguzo ya Moto, ambaye hujitangaza na kujitambuilisha kwamba Ndiye aliye Yeye, nasi tunamwamini,

jalia amzingire kila mtu humu ndani leo hii. Waponye wagonjwa. Wajaze kwa Roho. Tupe ukombozi kwa kila hali, Bwana, tunavyouhitaji. Iloweshe mioyo yetu kwa imani, Mungu, kwa imani isiyokufa, kwa imani imara kwamba tuna BWANA ASEMA HIVI. Tujalie, Bwana.

281 Ni watu Wako, Ujumbe Wako, Neno Lako, watumishi Wako. Na ibilisi hawezi kutushikilia. Hata hawezi kutuangamiza wakati maskani hii itakapoangamizwa. "Kwa maana kama maskani hii iliyo ya dunia ikiangamizwa, tunayo moja inayotungojea." Hawezi kutudhuru, kwa kuwa kila kitu kilicho adui yetu ni adui Yako, kwa kuwa sisi ni Wako. Tumenunuliwa kwa gharama, ya Damu ya thamani ya Yesu.

Kwa hiyo, ninyi pepo ambao mmewafunga watu hawa kwa maradhi, ninawaapisha, katika Jina la Yesu Kristo, mumtoke kila mmoja wao. Kama mtumishi wa Mungu, nikidai Neno hili kwamba ni Kweli, waacheni. Hamna haki. Kila kitu mlichopata kudai kwamba mnacho, kilibatilishwa pale Kalvari. Wala hamwezi kuwashikilia tena.

282 Sasa, Mungu, mpe kila mwanamume na mwanamke, mvulana ama msichana humu ndani, imani ya kuamini jambo hilo. Neno limenenwa. "Ukiuambia mlima huu, 'Ng'oka,' wala usitie shaka moyoni mwako." "Maombi ya imani humwokoa mgonjwa." "Utapata ulichoomba." Tunajua hilo. Tuna matumaini hayo kwa Mungu. Kama kweli tuna imani yoyote, kama Mungu anaishi ndani yetu, tunaamini hilo. Nami ninajua ndivyo ilivyo, Bwana. Kwa hiyo, tujalie, leo, kwa ajili ya maradhi na wokovu. Ama, hapana budi nilisema, ama nilipaswa kusema, wokovu kwanza halafu maradhi. Tujalie, Bwana, maana nafsi ina thamani zaidi kuliko mwili.

283 Lakini hao ambao, wakati mwingine, nafsi yao imeokolewa, na maskini mwili huu wa kale ungali ni mali ya Shetani, naye anajua ya kwamba atauchukua katika wakati wa mwisho. Ataupondaponda na kuurudisha. Mabuu ya duniani yatapenya ndani yake na kuula. Bali kamwe hayataigusa nafsi hiyo, kwa kuwa ndiyo hazina ya thamani ya Mungu. Na kupitia kwa uhai huo, kama vile kutoka kwenye jani, unarudi kwa Mungu aliyeutoa; utatokea kwenye msimu ufuatao, ukiwa na mwili mpya ambao Shetani hawezi kamwe kuugusa. Wala uzee wala chochote kile kisingeweza kuugusa. Utakuwa ni mwili wenye utukufu. Tunautazamia huo, Bwana. Wabariki watu Wako sasa. Hao ni Wako. Nami ninawakabidhi mkononi Mwako. Ninaomba haya katika Jina la Yesu.

[Ndugu Neville anatoa unabii—Mh.] Utukufu . . . Asifiwe . . . [Ndugu mwingine anatabiri.]

284 Hilo si neno langu. Hilo ni Neno Lake. Loo, tunachohitaji, majira haya, majira haya tunayoishi! Hivi hamfahamu, enyi marafiki, ya kwamba Mungu haji kwa watu mashuhuri? Yeye

huishi miongoni mwa walio wanyenyekevu, mambo madogo, duni. Huenda ikawa hamtambui kinachoendelea sasa hivi, kile kinachopitia kwenye jengo hili, kile kinachopitia miongoni mwa watu hawa sasa hivi.

285 Ni kwa nini Roho akasema, mapema, "Kabla sijawafanyia chochote," kupitia Ndugu Higginbotham? "Uangalieni Ujumbe huu, kwa kuwa nimeuleta," kitu kama hicho, "kuwaonya juu ya jambo hili linalokuja." Angalia kilichotukia.

286 Mambo mengine, Maandiko niliyokuwa nimeyaandika hapa chini, hata sikuyagusa, nikayaondokea kwa mbali. Niliongozwa huko nje na Roho Mtakatifu. Mnaona? Baadhi ya Maandiko, hata sikuyagusa. Nilienda tu kando kwenye jambo lingine, kabisa. Mara kwa mara, nikisikia kitu fulani kikija, mimi nageuka na kuona mahali kilipokuwa. Roho akinena katika kila upande sasa.

287 Loo, enyi watu, iweni wakweli, iweni waaminifu. Msijaribu kutegemea ninii. . .Mnaona, mna—mnatazamia kitu fulani kikubwa na kinachometameta.

Wakati, manabii wote, hata Daudi alisema, "Katika kule Kuja kwa Bwana, ya kwamba, kila mlima utashushwa, na—na mabonde yatainuliwa." Kasema, "Milima itaruka kama kondoo wadogo wa kiume, na majani yote yatapiga makofi yao." Vema, watu walifikiri hiyo ingekuwa ni nini, wakati Yesu alipokuja?

Ilitokea kuwa nini? Maskini mhubiri mnyenyekevu, hakuwa na elimu. Kwenye umri wa miaka tisa, aliingia nyikani, sio akafundishwe na mwanadamu, bali aka—akafundishwe na Mungu. Akatoka, na kusimama amejizungushia kipande cha ngozi ya kondoo, huku uso wake umejaa sufu, manyoya kila mahali, na nywele zimening'inia shingoni mwake. Akiishi huko nyikani, akila nzige, hao ni panzi, nzige wa mwitu na asali, wakati alipoishi nyikani. Basi akaja, akasimama kwenye matope ufukoni, na kutangaza kuja kwa Masihi. Ndipo Masihi akashuka akaja moja kwa moja, Mtu wa kawaida miongoni mwa watu, na akabatizwa. Nao manabii wote wakalitangaza kuwa ni moja ya mambo makuu sana yaliyopata kutukia, nalo lilikuwa hivyo. Mnaona?

288 Wanatazamia kitu fulani kikuu, kinachong'aa, kutukia. Mnaona? Roho Mtakatifu hang'ai. Yeye humeka. Kung'aa ni kwa ulimwengu. Kumeka ni kwa Mungu.

Nimekee, Bwana, ndilo ombi langu. Ninyenyekeze kabisa. Nitwae, nifinyange na unifanye. Roho wa Mungu aliye hai, tenda kazi upya juu yangu. Nifinyange, nifanye. Nifanye kuwa Wako, Bwana. Nitwae tu.

289 Ninajua tu ya kwamba Roho wa Kristo anatembea kwenye jengo hili hapa asubuhi ya leo. Mungu yule atakayeuhukumu ulimwengu yupo papa hapa sasa, kwa hakika tu kama ninavyosimama kwenye mimbara hii. Kumekuwako na

thibitisho moja, mawili, matatu yake, ya Neno, vile vile hasa Biblia ilivyosema. Mliisikia ikinyamaza wakati huo, baada ya hapo? Moja, mbili, tatu, kila kitu katika utaratibu wa kiroho, kila kitu katika utaratibu wa Kimaandiko. Loo, ifungueni mioyo yenu na mfahamu. Loo, wakati mzuri jinsi hii, ni kitu gani kingeweza kutukia kwenye wakati huu!

290 Walikuwa kwenye chumba cha juu, wote wakiwa katika nia moja, wakingojea. "Kwa kuwa hao wamngojeao Bwana watapata nguvu mpya. Watapanda juu kwa mabawa kama tai."

291 Usipande tu kwenda huko na kusema, "Bwana, nasikitika, dhambi zangu. Sasa nakubali kwa imani ya kwamba ninaye Roho Mtakatifu," na uende zako.

Wale wamngojeao Bwana, majuma, siku kadhaa, chochote kile, watapata nguvu mpya. Watapaa juu kwa mabawa ya tai. Watapiga mbio wala hawatachoka. Kama wakienda kwa miguu, hawatachoka. "Nifundishe, Bwana. Nifundishe, Bwana, kungoja." Mngojee Bwana.

292 Mchana na usiku, daima, Hana alikuwa hekaluni, akiomba daima, mchana na usiku. Walipomleta Yesu. Yeye aliingia, kipofu, kwenye hilo jengo, akajongea huku na huku. Mwanamke kipofu akaweka mikono yake juu Yake na kumbariki Mungu. Kwa kuwa, katika upofu wake wa kimwili, rohoni mwake, yeye aliongozwa na Roho, mpaka mahali alipokuwa amesimama.

293 Hapo, Simeoni, akimngojea, huko nyuma kwenye chumba cha kuombea huko nyuma, alijua ya kwamba alikuwa na ahadi, kwa Roho Mtakatifu, ya kwamba asingekufa; mzee, mwenye umri wa miaka themanini, karibu tisini. Naye alikuwa . . . aliwaambia watu waziwazi, "Sitaona mauti mpaka nitakapomwona Masihi." Na kwenye dakika ile ile, maskini Mtoto mchanga . . .

Alikuwa ni Nani? Sio mtu mashuhuri, walinzi wote wamesimama miguu sawa wakati walipomleta Masihi humo ndani, amevikwa vizuri sana na anapendeza, na ni mzuri na amerembeshwa, na kutiwa manukato kama watoto wachanga wanaokuja kuwekwa wakfu. Lakini maskini mama mdogo aliyekuwa amesengenywa, kasema, "Alimzaa Mtoto, nje ya ndoa takatifu." Amevikwa nguo za kitoto, za maksai, amezungushiwa vitambaa vya maksai, akitembea humo jengoni, na kila mtu akimwepa.

Lakini hili hapa kundi hilo dogo linakuja, kundi hilo dogo. Hana, akiwa ni mmoja wao. Mwingine, ni Simeoni, akishuka kupitia mstarini, pasipo kujua ni lini atakapomwona Huyo. Ndipo akainua mikono yake na kusema, "Bwana, mruhusu mtumishi Wako aondoke kwa amani sasa, kulingana na Neno Lako, kwa kuwa macho yangu yanauona wokovu Wako." En-he. Mnaona? Sio kitu kikuu, kinachong'aa. Ni mmeko; na ingawa inatajwa kwa ubaya, ilikuwa ni ishara.

294 Na, leo hii, ishara hiyo inatajwa kwa ubaya. Haina ushirikiano. Ni—Ni. . . .Inatukanwa, na kuitwa kila kitu. Bali ni ishara inayopuuzwa, ishara inayotukanwa. Biblia inanena juu ya hilo, “Ishara, inayotajwa kwa ubaya.”

295 Na tukumbuke hili tunapoenda manyumbani mwetu. Kamwe msiuache Ujumbe huu ufe kutoka mioyoni mwenu. Lolote mfanyalo, kamwe msifanye hivyo. Litafakarini Hili, mchana na usiku. Na muombe, mchana na usiku, kwamba Mungu amwinue shahidi Wake sasa. Tuko tayari, kwa kuwa ninaamini, hivi karibuni, hakutakuwako na wakati tena. Tunakuja.

296 “Vipi, itakuwa ni lini, Ndugu Branham?” Sijui. Labda leo. Huenda ikawa ni kesho. Kama si leo, nitalitarajia kesho. Na huenda ikawa ni mwaka huu, mwaka ujao, miaka kumi. Labda miaka thelathini, sijui itakuwa ni lini. Lakini ninasema, tangu sasa na kuendelea, iweni tayari kila dakika.

297 Na usichukue kitu fulani tu vivi hivi. Usifanye hivyo. Kamwe usipumzike, mchana na usiku, mpaka umezungumza na Mungu. Jiepushe na ushupavu. Usishikwe na mhemko. Usifanye hivyo. Huo ndio unaoleta ulokole uliokithiri na huwafanya watu wauogope, mnaona, ni kwa sababu ya ulokole uliovuka mpaka. Usikubali hilo; hata kidogo. Wewe kaa papo hapo mpaka utakaponena na Mungu. Hata hivyo, ni nafsi yako, na wewe ndiwe unaenda kwenye Umilele huko ng’ambo. Na uwe na hakika kwamba hupeani tu mikono na kukariri kanuni za imani, au—au kukubali kitu fulani kwa imani. Usifanye hivyo. Wewe zungumza na Mungu. Acha Mungu aseme nawe, ndipo uangalie litakalotukia kwako. Angalia shauku zako na kile kitakachotukia, ndipo utajua kama ulinena na Mungu ama sivyo.

298 Kwenu ninyi ambao mmemwamini asubuhi ya leo. Kwenu, na mimi—mimi nilisema kuhusu miito ya madhabahuni. Je! mnajua jinsi walivyofanya jambo hilo katika Biblia? “Wote waliomwamini Bwana, wote waliomwamini Bwana walibatizwa katika Jina la Yesu Kristo wapate ondoleo la dhambi zao.” Ikiwa kamwe hujaninii. . .Kamwe hatukuwa na miito ya madhabahuni. Kamwe hawakuwaacha watu waje huku. Unapofanya hivyo, unapata kila kitu. Huyu hapa jamaa fulani anakuja madhabahuni, anayeonekana mwenye kiburi, na kupiga magoti, kwa sababu mtu fulani alijaribu kumpata. U—u—utapata shida maradufu kumpata tena. Unaona? Nawe unafanya nini? Unapata kila kitu humo. Naye Yesu alisema, “Wote alionipa Baba watakuja Kwangu.” Dumu na Neno hilo. Mungu atafanya yaliyosalia. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Mungu atafanya yaliyosalia.

299 Mungu awabariki. Ninatumaini kuwaona tena usiku wa leo, natumaini, kila mmoja wenu awezaye. Ninajua wengi wenu

inawabidi kukaa nje, mbali. Nitakuja usiku wa leo, kumsikiliza ndugu yangu, kama yakiwa ni mapenzi ya Mungu. Sitaki kuchukua jumbe zake zote mbili.

300 Na—naye Ndugu Neville ni mtu mzuri wa Mungu. Nami ninajua, ninajua ni nani. . . Ninapomsikia akihubiri, ninajua yanatoka moja kwa moja kutoka moyoni mwake. Ninajua hilo. Naye Ndugu Neville, kama alivyosema hivi majuzi usiku, tamshi lile, kasema nilitoa tamshi. "Siku moja nitambatiza katika Jina la Yesu." Nilimbatiza. Kwa nini? Niliona uaminifu na ukweli ndani yake. Nilijua kama yeye. . . angaliweza tu kupewa, na nikaona yeye. . . na yeye—yeye angeweza kuliona kweli, macho yake yangefumbuliwa, angeweza kulipokea. Nikangojea, na kuliambia Kanisa, "Msijali, huyo mhubiri wa Kimethodisti atakuja tu." Naye huyu hapa leo hii, mchungaji wa maskani hii, imara tu katika huduma awezavyo kuwa, katika Ujumbe. Yeye anamwamini Mungu. Nami ninajua, ninaposikia jambo fulani likitoka kwa Ndugu Neville, ninajua ni halisi, linatoka kwa Mungu, kwa kuwa yeye ni mtu wa namna hiyo.

301 Nimeiweka mikono yangu juu ya leso zenu hapa ambazo zimeombewa. Nikitumaini, kila mmoja wenu amepokea baraka kutoka kwa Mungu. Ninatumaini Mungu yumo mioyoni mwenu.

302 Hatu—hatuji hapa ku—kupata baraka kutoka kwa Mungu, sana, jinsi tunavyokuja hapa. Kila siku tunapopumua pumzi, tunapata baraka toka kwa Mungu. Kile kinachotuleta hapa, ni kusahihishwa, kukatilia mbali, kuitahiri mioyo yetu, na kuja uweponi mwa Mungu, na kumwamini Mungu kwa mioyo yetu yote.

303 Kumbukeni Neno la Bwana. Na msisahau, wala kushindwa, kuiangalia ishara ya kweli iliyotumwa kutoka kwa Mungu.

Halafu nitairudisha ibada kwa Ndugu Neville, nimwache aseme lolote analotaka kusema.

[Ndugu Branham anaondoka mimbarani, naye Ndugu Neville anasema, "Mimi hakika, jamani, ninawaambia, ninajua kwamba Mungu alithibitisha kile tulichotarajia mwanzoni mwa ibada. Ninapoangalia kwenye nyuso hizi nyingi, asubuhi ya leo, ninajua imekuwa ni vema kwamba mmekuwa hapa. Na imekuwa vema kwamba nami nimekuwa hapa. Nami nilipaswa kuwa hapa, nanyi mlipaswa kuwa hapa. Azma yenu imetimizwa vizuri kabisa kama mkiihesabu kuwa imetimizwa. Mlicho nacho asubuhi ya leo, mnaweza kuwa nacho kwa kuwa mlikipokea kutoka kwa Mungu. Na mara moja tutakuwa na ibada ya ubatizo, baada ya hapa. Naye Ndugu Willard Collins ataiongoza ibada ya ubatizo, nasi tuna watu wawili ama zaidi. Nasi tungetaka kuona watu mia moja wa kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo, asubuhi ya leo."—Mh.] Amina! ["Yakinia kuonyesha imani yako kwa njia dhahiri. Imani kamwe siyo matendo. Imani, ya mdomoni, haifai kitu. Bali imani, iliyodhihirishwa, ndiyo

utaratibu wa Biblia."] Amina! Hiyo ni kweli. ["Kupitia utii, imani inaweza kuonyeshwa. Mungu na amjalie mtu yeyote, asubuhi ya leo, aliyepo hapa, anayejisikia akiongozwa kufanya hivyo, naomba uje. Kama hii ni ninii. . . Kama hii kidogo ni nje ya utaratibu wa yale uliyokuwa umepanga, ama labda ulikuwa na miadi ya kufanya mara moja, ama chochote kile, kama unaweza kuiahirisha hiyo, na kumalizana na tendo hili la utii; ninaamini kama ndugu yenu mnyenyekevu katika Kristo, na kama mfanya kazi mwenza pamoja na nabii wa Mungu, ninaamini lingekuwa—lingekuwa ndilo chaguo lako lililo bora kuliko yote, kufanya uamuzi huo sasa."] Mungu na alijalie. . .?. . .["Na iwe kwamba utakuja, na kupachukua mahali pako miongoni mwa wengine ambao watabatizwa, upate kuwa kwenye hesabu hii, inayojumuisha kundi hili dogo. Loo, ni ajabu, sivyo, kuwa mmoja Wake, na kuwa kulingana na Neno Lake? Naomba sisi sote tusimame pamoja, tunapojiandaa kufumukana. Jumapili ijayo, Ndugu Branham atakuwa pamoja nasi tena. Hebu na tulikumbuke tangazo hilo. Yeye alisema angekuwa huku usiku wa leo, bali hakusema angehudumu. Hata hivyo, shauku yangu ni, daima, ya kwamba angehudumu. Naye hana haja kuwa na hofu kuhusu msimamo wangu juu ya hilo. Shauku yangu haina shaka kabisa, nikijua ya kwamba Ujumbe na wi—wito, wadhifa alio nao, unahitajika sana katika siku hii ya mwisho. Ninatoa nafasi, wakati wowote. Nitasema jambo hili mbele za watu na yeye. Mimi, kwa furaha nitatoa nafasi, wakati wowote, kwenye ibada yoyote, kwa ajili ya Ujumbe huu muhimu ninaouamini. Kwa kuwa, Mungu alinena kupitia sisi wawili, asubuhi ya leo, akionyesha ishara ya jambo hili. Nami ninafurahi sana kuwa na majaliwa ya kuweza kuwa ni mtu tu ambaye anaweza kumpa nafasi. Nami ningeninii, usiku wa leo, kwamba ningefurahi, kama ndugu yetu, na mtumishi wa Mungu na nabii, alitaka kufanya hivyo, kwa furaha sana nitampa nafasi. Akisema tu, lolote analojisikia. Lakini, yeye amenena, nasi tutaweka tu uamuzi wa jambo hilo lote mikononi mwa Mwenyezi Mungu." Ndugu Branham anarudi mimbarani—Mh.]

304 Usingeweza kuomba jambo lililo zuri zaidi, sivyo, kutoka kwa ndugu halisi? Sababu ya mimi. . . Mnaona, marafiki, ni—ninajua mnanipenda. Mnampenda Ndugu Neville. Mnawapenda watu wote wa Mungu. Tunapendana mmoja na mwingine. Kama kulikuwako na wakati ambapo tunapaswa kupendana, ni leo hii. Inatupasa kupendana sana, ndugu, hata tuninii tu. . . Tungekuwa halisi sana kuliko ndugu na dada wa kuzaliwa. Huo ndio upendo unaopaswa kuwa mioyoni mwetu mmoja kwa mwingine, kicho na heshima, iliyo ya juu sana. Nami ninapenda hilo. Ninapenda kitu hicho kilicho halisi.

305 Na hapa, Ndugu Neville, na Ndugu Higginbotham. Ndugu, ninaamini huyo alikuwa ni Ndugu Funk. Hata haikusikika kama ni yeye, aliyetoa ujumbe huo huko nyuma, uliokuja. Zilitoka kwa

Mungu, jumbe hizo, enyi marafiki. Ni kweli kabisa. Mtu yeyote aliye na utambuzi wa kiroho anajua hilo.

306 Lakini mambo yako hivi. Katika kuja, ni—ninampenda Ndugu Neville sana mpaka ninawazia hili, mnaona. Si—sipendi kusema jambo lolote 'sipokuwa kweli niwe na jambo fulani kutoka kwa Mungu kuwaambieni. Mnaona? Nami nilikuwa na huu—huu ulikuja moyoni mwangu, yapata siku mbili ama tatu zilizopita, nami sikupata nafasi ya kuuangalia sana mpaka jana usiku, kufuatilia Maandiko machache. Hiyo ndiyo sababu nilikuja kuuleta. Umetoka mikononi mwangu sasa. Mnaona? Lolote mtakalofanya nao, hiyo ni juu yenu, hiyo itakuwa ni shauri yenu, mnaona. Bali umetoka mkononi mwangu.

307 Lakini, mimi pamoja na Ndugu Neville, tuko hivyo tu. Nikishuka kuja hapa, kuninii tu—kuzungumza tu wakati mwingine, na kitu kama hicho, naye Ndugu Neville alikuwa na ujumbe kutoka kwa Mungu, ningeketi papa hapa chini. Kweli, kabisa. Ningetoa nafasi kwa ajili ya ujumbe wa Mungu, daima. Mnaona? Hivyo ndivyo tunavyofanyiana mmoja kwa mwingine. Hiyo ndiyo sababu ninasema nitaninii . . . Kama—kama Mungu hatanipa chochote, basi, labda, kuzungumza tu. Na kama Mungu akimpa Ndugu Neville chochote, nami niko papa hapa mimbarani, Jumapili asubuhi, Jumapili usiku, wakati wowote ule, Ndugu Neville angeninii tu . . . Angekuwa ni ndugu kutosha. Angenijia, aseme, "Ndugu Branham, ninaamini wewe ni mtumishi wa Mungu, bali Mungu ndiyo kwanza anipe ujumbe." Ungefanya hivyo, sivyo? [Ndugu Neville anasema, "Amina."—Mh.] Naam, bwana.

308 Ningemfanyia vivyo hivyo, kama alikuwa anataka kuzungumza. Ningesema, "Ndugu Neville, utaniwia radhi? Mungu amenipa ujumbe. Sina budi kuutoa kwa watu, sasa hivi." Naye, Ndugu Neville, atanipa nafasi moja kwa moja; yeyote wetu, mmoja kwa mwingine. Mnaona? Hivyo ndivyo tunavyofanya. Na basi kama sisi, endapo sina jambo maalum, basi ninaninii . . .

309 Ninapenda tu kumsikiliza akihubiri. Nilimsikia. Ni wangapi waliomsikia, Jumapili iliyopita usiku? Ujumbe mzuri kama huo, nawaambia. Ulishikamana kabisa, yale yaliyosemwa asubuhi.

Na, enyi watu, ninawaambia, mna Neno la Mungu la kutosha hata mnapaswa kuishi vizuri na mwe wazuri.

Bwana akubariki sasa, Ndugu Neville.

*Ishara Ya Kweli Iliyopuuzwa* SWA61-1112
(A True Sign That's Overlooked)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, tarehe 12 Novemba, 1961, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings.

SWAHILI

©2018 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.


Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:


VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org